# Nipashe

Jumatatu Mei 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580228

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Sido ya JPM ilivyomtengenezea viwanda 4,500 na ajira maelfu

UKURASA 4




UKURASA 11

**UBUNGE WA MWAMBE**

# Shirika kumshtaki Ndugai Korti Kuu

**NI** baada ya spika huyo kutupa barua ya Chadema iliyomtaka... *Endelea ukurasa 2*



Spika Job Ndugai



## BAA LA CORONA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetoa takwimu mpya za virusi vya corona duniani. Kwa mujibu wa takwimu za jana, watu 3,865788 wamepata maambukizo wakati vifo ni 265,862. Kwa Afrika, maambukizo 40,554 na vifo 1,322,000. Kuosha mikono mara kwa mara na kuepuka mikusanyiko ni mambo ya kuzingatiwa kila siku.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## OFISI ARDHI MIKOA RASMI

UKURASA 2

## Zanzibar yaibua tena hoja ya kujiunga OIC

UKURASA 17




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** SINGIDA UTD YATAKA LIGI KUU BARA IFUTWE UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

# Shirika kumshtaki Ndugai korti kuu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

SHIRIKA la Uraia na Msaada wa Sheria (Cilao), limesema kuwa kwa kushirikiana na wadau wengine, linakusudia kufungua kesi Mahakama Kuu, kuomba ufafanuzi wa mahakama hiyo kuhusu kitendo cha Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuruhusu Cecil Mwambe kushiriki shughuli za Bunge ilhali amepoteza sifa za ubunge.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Cilao, Odero Odero, shirika hilo limesikitishwa na kitendo cha Spika kuchukua uamuzi huo, likidai unakiuka misingi ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Itakumbukwa kwamba, Bunge na vyama vya siasa vinaongozwa kwa mujibu wa katiba na sheria zingine za nchi. Ibara ya 71 ya katiba ya nchi inaeleza wazi kuhusu ukomo wa mtu kuwa mbunge.

"Kwa mujibu wa ibara ya 71(1)(e) ya katiba, ni wazi kuwa mbunge atapoteza nafasi yake ya ubunge ikiwa atapoteza uanachama wa chama chake kilichompatia udhamini wakati wa uchaguzi," shirika hilo lilisema katika taarifa yake hiyo.

Shirika hilo lilikumbusha kuwa Mei 6 mwaka huu, Spika Ndugai alimruhusu Mwambe kushiriki shughuli za Bunge, licha ya mwanasiasa huyo kutangaza hivi karibuni kujiuzulu nafasi yake ya ubunge kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Lilisema kuwa Mwambe, aliyekuwa Mbunge wa Ndanda mkoani Mtwara, alitangaza uamuzi wake huo na kuweka bayana kwamba anajiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Mwambe alitangaza kujiondoa Chadema, basi tunaamini pasipokuwa na shaka, amepoteza sifa ya kuendelea kuwa mbunge," shirika hilo lilisema katika taarifa yake hiyo.

Lilisema kitendo cha Spika Ndugai kumruhusu Mwambe kuendelea kushiriki shughuli za Bunge ni ukiukwaji wa katiba ya nchi.

Shirika hilo lilisema kwa kuwa katiba inatamka wazi katika ibara ya 26(1) kuwa kila raia ana wajibu wa kusimamia na kutetea katiba na sheria, litashirikiana na wadau wengine katika kusudio lake hilo la kufungua kesi Mahakama Kuu kuomba ufafanuzi wa mahakama kuhusu kitendo hicho cha Spika Ndugai.

Wiki iliyopita, Spika Ndugai alitangaza bungeni kuwa hajaridhishwa na barua iliyoandikwa na Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, kwa Spika kuhusu kuzuia Mwambe kushiriki shughuli za Bunge na kulipwa na chombo hicho cha kutunga sheria. Spika Ndugai pia alisema hajapokea barua ya Mwambe kujivua uanachama wa Chadema na kujiuzulu ubunge wake, hivyo hata barua ya Mnyika kwake haina mashiko kwa sababu haikuambatanishwa barua ya Mwambe kujiuzulu ubunge na uanachama wa Chadema.

Siku chache baada ya kauli hiyo ya Spika, Mwambe alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa ameitika wito wa Spika na atakwenda bungeni kushiriki shughuli za chombo hicho.

## Maji yazingira makazi kando Ziwa Victoria

**Na Enock Charles**

WAKAZI wanaoishi karibu na fukwe za Ziwa Victoria Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, wamehama makazi yao baada ya maji kujaa ziwani na kuingia kwenye nyumba zao.

Aidha, maji hayo yamesomba vitu mbalimbali vya wakazi hao, zikiwamo samani.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari nchini, Diwani wa Kata ya Miembeni, Richard Gasper, alieleza kuwa katika Mtaa wa Nyamkazi nyumba zaidi ya 280 zimeathirika na maji na kuwaacha wakazi wake hao bila makazi.

"Tumeathirika, kaya zaidi ya 280 zimeshahama mtaa huu na kwenda maeneo ya jirani, kwa hiyo hali sio nzuri, upepo ukipiga maji yanapanda juu," alisema.

Alisema kwa sasa kuna hofu kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo kuathirika zaidi kutokana na makazi yao kujaa maji, hivyo kusababisha watu kupoteza mali na makazi. Aliwaomba wananchi wa mitaa ya jirani kutokuwapandishia kodi watu walioathirika na kadhia hiyo na kwenda kutafuta makazi katika maeneo yao.

Naye Neema Salvatory, mkazi wa Nyamkazi, alisema kujaa kwa maji hayo na kuingilia makazi yao kumemwathiri kibiashara baada ya watu kuyahama makazi yao, hivyo kusababisha upungufu wa wateja.

"Katika biashara yetu sisi tulikuwa na uwezo wa kutengeneza mpaka Sh. 90,000 kwa siku, lakini hivi sasa tunapata hadi Sh. 20,000... ni kutokana na watu kukimbia, wafanyabiashara wa samaki na dagaa wenyewe nao wamekosa sehemu ya kuanika dagaa zao," alisema Neema.

Kiwango cha maji katika Ziwa Victoria kimeripotiwa kuongezeka, hivyo kuwatishia wakazi waliojenga nyumba karibu na ziwa.




Watendaji wa Sekta ya Ardhi, Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Tanga wakiwa wamesimama katika bango la kutambulisha ofisi ya mkoa huo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Ofisi za ardhi mikoa kuanza mwezi huu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

OFISI za ardhi za mikoa zitaanza rasmi kufanya kazi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara mwezi huu.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli kuitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuondoa kero na mzigo wa gharama kwa wananchi katika masuala ya ardhi.

Uanzishaji ofisi hizo ni usogezaji huduma za sekta ya ardhi karibu na wananchi sambamba na kuwapunguzia gharama za kufuata huduma hiyo umbali mrefu, ambapo huduma za ardhi awali zilikuwa zikitolewa kwenye ofisi za Ardhi za Kanda na Makao Makuu.

Akizungumza jana jijini Dodoma kabla ya kuwasilisha makadirio ya hotuba yake hapo leo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema wizara imeanzisha ofisi za ardhi katika kila mkoa ili kutoa huduma zote zilizokuwa zinatolewa kwenye ofisi za kanda au makao makuu.

Alisema, kuanzia sasa wananchi watapata huduma zote ndani ya mikoa yao, na kubainisha kuwa wananchi wa mikoa ya Kigoma na Katavi hawataenda tena Tabora kuchukua hati kama walivyokuwa wakifanya awali huku wale wa Tanga, Manyara na Arusha wakipata huduma katika mikoa yao badala ya kwenda Moshi na wale wa mikoa ya Iringa, Njombe, na Rukwa wakisalia mikoa husika badala ya kwenda Mbeya.

Aidha, wananchi wa mikoa ya Ruvuma na Lindi sasa hawataenda mkoa wa Mtwara kupata huduma za ardhi na wananchi wa Kagera na Geita nao hawatalazimika kwenda Mwanza, huku wa mikoa ya Mara na Shinyanga wakisalia mikoa yao kupata huduma za ardhi, hivyo hawataenda Simiyu na wale wa Singida na Morogoro wakiepuka kwenda mkoa wa Dodoma kuchukua hati.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, nyaraka zote, watumishi pamoja na vitendea kazi tayari vipo mikoani na kubainisha kuwa sasa taasisi kama benki zitaweza kukopesha kwa kasi kwa kuwa dhamana za wakopeshwaji (Hati) zipo mikoani na masjala za hati zimerudishwa kila mkoa.

Waziri alisema wasajili wa hati wa mikoa watatoa hati kwa wananchi kupitia ofisi za ardhi za wilaya badala ya wananchi kufuata hati kwenye kanda au mkoani, na kuongeza kuwa, vifaa vya upimaji vimenunuliwa na kusambazwa ofisi hizo za mikoa ili halmashauri za wilaya ziweze kuazima na kupima maeneo yao bila gharama za kuvikodisha.

"Tumeanza mkakati wa kununua vifaa kwa kila wilaya. Uanzishwaji wa ofisi hizi ni utekelezaji wa maagizo ya Mhe. Rais aliyetutaka tuondoe kero na mzigo wa gharama kwa wananchi na wadau mbalimbali wa ardhi," alisema Lukuvi.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa (katikati), akimkabidhi vifaa vya kinga dhidi ya corona Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Daudi Mayeje, kulia ni Meneja wa Mwafrika Phamancy. Msaada huo umetolewa na duka la dawa za binadamu Mwafrika Phamancy wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni mbili. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Jaji amwachia huru mshtakiwa wa mauaji

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Kigoma imemwachia huru mkazi wa Kijiji cha Mkongoro Wilaya ya Kigoma, Idrisa Hamimu (31), ambaye alikuwa ameshtakiwa kwa kosa la kumuua mama yake wa kambo.

Hamidu alishtakiwa kwa kosa la kumuua Halima Ntibaluta kwa kumpiga na jembe kichwani, begani na tumboni na kufariki dunia.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama hiyo, Athumani Matuma, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa hilo.

Alisema shahidi namba moja alisema tukio hilo lilitokea Machi 21 mwaka 2012 majira ya saa 12:30 jioni katika Kijiji cha Mkongora Wilaya ya Kigoma walikuwa nyumbani na wenzake wakizungumza, lakini mama yake mshtakiwa alikuwa ameachana na baba yake mshtakiwa, kwa hiyo mshtakiwa alikuwa akiishi na mama wawili wa kambo.

Aidha, alisema wakati wakiwa hapo nyumbani siku ya tukio majira ya saa 12:30 jioni mshtakiwa alifika nyumbani na kuchukua jembe na kuanza kumpiga mama yake Halima kichwani, begani na tumboni, na kuwa baada ya tukio hilo mama huyo alipelekwa hospitali na wakati akipatiwa matibabu, alifariki dunia.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Riziki Matitu na upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa kujitegemea, Sylvester Damasi.

Alisema shahidi namba tatu wa upande wa mashtaka alidai siku ya tukio alikuwapo nyumbani na alimuona mshtakiwa kwenye tuta la maharage akimpiga na jembe marehemu kichwani, tumboni na begani, na kuwa alimrushia fimbo mshtakiwa ili asimpige marehemu.

Aidha alisema mashahidi wa upande wa mashtaka wanapingana sana, tena walijichanganya sana, hivyo mahakama kushindwa imwamini nani katika mashahidi hao watatu wa upande wa mashtaka.

Alisema shahidi namba moja na namba tatu hawakuona wala hawajui mshtakiwa alikamatiwa wapi?

Jaji Matuma alisema baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake, lazima Mahakama ifanye uamuzi mdogo wa kuona kama mshtakiwa ana kesi ya kujibu au la, lakini katika kesi hiyo ya mauaji Mahakama inaona mshtakiwa hana kesi ya kujibu kwa sababu mashahidi wa upande wa mashtaka wameshindwa kuthibitisha kosa hilo.

Alisema kwa kuwa upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa hilo, Mahakama inampa nafuu mshtakiwa kwa sababu upande wa mashtaka una kazi ya kuthibitisha kosa pasipokuacha shaka yoyote sasa.

Jaji Matuma alisisitiza kuwa upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa la mauaji.

"Mimi kwa akili yangu nimeona upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa hili, kifungu cha 293(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 Marejeo ya mwaka 2019, mshtakiwa hana hatia, hivyo namuachia huru, na haki ya rufani ipo wazi," alisema jaji huyo.

Awali akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali Mwandamizi, Riziki Matitu, alidai kuwa Machi 21 mwaka 2012 majira ya saa 12:30 jioni katika Kijiji cha Mkongoro Wilaya ya Kigoma, mshtakiwa alimuua Halima Ntibaluta kwa kumpiga na jembe kichwani, begani na tumboni na kumsababishia kifo.

# Wanaokaa kwenye makundi vijiweni watangaziwa kiama

**Na Yasmine Protace, KIBITI**

KATIKA jitihada za kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, imetangaza hatua ambazo zitachukuliwa kwa watu ambao watakamatwa wakiwa wamekaa vijiweni katika makundi.

Moja ya hatua hizo ni kukamatwa na kupelekwa kufanya shughuli za usafi.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Gulam Musini Kifu, katika kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa corona, kila mtu anatakiwa kuchukua hatua za kujilinda na kuwalinda wengine dhidi ya maambukizo.

Kifu alisema baadhi ya watu bado wanakaa vijiweni na kuendeleza mikusanyiko ambayo imekatazwa.

"Kutokana na watu kutosikia makatazo ambayo serikali inatutangazia kila siku katika kujikinga na corona, kwa Kibiti nimeshamwambia OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) wakiwakuta vijana vijiweni wawakamate, wawapeleke sokoni, ofisi ya mkurugenzi, kituo cha Polisi na hospitali wakafanye usafi ikifika jioni wawaachie waende makwao," alisema.

Aliongeza kuwa kuwafanyisha usafi kila wanapokamatwa, hatua hiyo itasaidia kupunguza mikusanyiko ambayo haina faida.

Pia aliwataka madiwani pamoja na kamati ya ulinzi na usalama kuwahamasisha wananchi kuhusu uvaaji wa barakoa, ikiwa ni moja ya hatua za kujilinda dhidi maambukizo ya virusi hivyo.

"Mnapoenda kuhamasisha wananchi uvaaji wa barakoa, hakikisheni na nyie mnaenda mkiwa mmevaa," alisisitiza Kifu.

# Bilioni 15/- zatengwa kukarabati barabara

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, amesema matengenezo ya dharura kwenye barabara na madaraja zinazoharibika kipindi cha mvua kubwa, yalitengewa Sh. bilioni 15 katika mwaka huu wa fedha.

Amesema kuwa katika Jimbo la Ushetu, tayari wameshatoa Sh. milioni 39 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za dharura zilizokuwa zimeharibika vibaya na kutopitika, huku akizishauri halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ambazo haziko kwenye mtandao wa barabara.

Kwandikwa ambaye ni Mbunge wa Ushetu, aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari katika Kijiji cha Mbika kuhusu ubovu wa barabara.

Alisema bado tatizo hili hasa maeneo ya vijijini, lakini Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) umepatiwa fedha kwa ajili ya maeneo yenye uhitaji wa dharura.

Kwandikwa alisema fedha zilizokuwa zimetengwa na serikali kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara, zimeshatumika katika maeneo mbalimbali nchini.

"Bajeti ya mwaka ujao, katika kutenga fedha, wizara tumeangalia hasa suala la fedha za dharura. Kwa mwaka huu unaoisha, tulitenga kiasi cha Sh. bilioni 15 kwa ajili ya dharura.

"Tumetengeneza madaraja mengi kama vile Daraja la Mto Mara, Manyara, Sibiti, Magufuli, Mombo na Busisi ikiwa ni sehemu ya mikakati ya wizara ambayo ilikuwa imejipanga vizuri kukabiliana na dharura za aina hiyo," alisema.

Kwandika aliongeza: "Kutokana na uharibifu mkubwa wa barabara kwenye baadhi ya maeneo, mfano Jimbo la Ushetu, tayari mkandarasi amekwishafanya usanifu, yupo kwenye eneo baada ya kupatiwa fedha ya matengenezo ya barabara inayotoka Ulowa hadi Ubagwe kwa kiwango cha changarawe na inayotoka Uyogo hadi Kahama Mjini yenye urefu wa kilomita 54 kwa kiwango cha lami.

Kwandikwa alisema kuwa wakala wa barabara nchini (Tanroads) umekuwa ukifanya vizuri, lakini barabara za maeneo ya vijijini ambazo zinatekelezwa na Tarura zimekumbwa na matatizo kipindi hiki cha mvua kubwa.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**DATE: 08th May 2020**

**ADDENDUM TO REQUEST FOR INVITATION TO BID (ITB) No. ITB/2020/SUP/024**

**FOR THE SUPPLY AND DELIVERY OF PHARMACEUTICALS**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Tanzania Representation office would like to draw your attention on the above invitation to **bid ITB/2020/SUP/024** for the supply and delivery of pharmaceuticals.

1. The submission deadline is extended to **13th May 2020 – 16:00** HRS EAT
2. Please note that all terms and conditions of the tender documents remain unchanged except change of the submission date above.
3. In case you require further details or clarifications, kindly contact ishobeza@unhcr.org

**Yohannes Hailu**
**Senior Supply Officer**
**UNHCR Representation Office Dar es Salaam**

157366

# Sido ya JPM yamtengenezea viwanda 4,500, ajira maelfu

## Zao la mikopo ya mabilioni sura '50/50'

**Na Enock Charles**

MAENDELEO ya ujasiriamali na viwanda vidogo ni chachu ya kutengeneza ajira sanjari na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, vikundi na taifa kwa ujumla.

Kwa kulitambua hilo, serikali ilianzisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO), ili kuwezesha uanzishwaji wa viwanda hivyo, kuvikuza na kutoa mchango wa uchumi wa taifa.

Sido ilianzishwa kwa sheria ya Bunge Na. 28 ya mwaka 1973, ikipewa majukumu kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuratibu, kukuza na kusaidia kutoa huduma mbalimbali kwa viwanda vidogo.

Ili kufahamu mchango wa shirika katika eneo hilo, Nipashe ilipata nafasi ya kuteta kwa faragha na Mkurugenzi Mkuu wa Sido, Profesa Sylvester Mpanduji.

Mkurugenzi Mkuu huyo anasema shirika hilo limepewa majukumu ya kuwezesha, kuanzisha, kukuza na kuendeleza viwanda vidogo nchini kwa manufaa ya taifa, msisitizo ukiwa kwenye kujenga, kubuni na kuendeleza ubunifu katika eneo la ujasiriamali kwa kuwajengea uwezo watu binafsi, vikundi na taasisi, ili kutoa mchango endelevu katika maendeleo ya taifa.

Abainisha kuwa katika awamu hii ya uongozi wa serikali, Sido inatekeleza mkakati wa uchumi wa viwanda ambao unalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda ifikapo mwaka 2025, ambapo mchango wa sekta ya uzalishaji mali katika uchumi wa taifa unatarajiwa kufikia asilimia 40 ya pato la taifa.

Prof. Mpanduji anasema ili kufikia malengo hayo, Tanzania inatarajia kubadili mfumo wake wa uchumi kutoka mfumo ambao kwa kiwango kikubwa unategemea mauzo ya bidhaa ghafi, utalii na madini na kwenda katika mfumo ambao uchumi utategemea zaidi mauzo ya bidhaa za viwandani ama zile za kilimo, lakini zikiwa tayari zimesindikwa na hivyo kuongeza thamani sokoni.

"Ili kuhakikisha lengo hilo linatimia, Sido sasa ina jukumu la kutambua, kutafuta na kusambaza teknolojia kwa ajili ya matumizi ya viwanda vidogo na vya kati.

"Utekelezaji katika eneo hili kwa miaka minne ya serikali hii, jumla ya teknolojia mpya 699 zilitambuliwa na kusambazwa. Teknolojia hizo ni za ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo na ukamuaji wa mafuta ya mawese.

"Vilevile, teknolojia za usindikaji wa vyakula, upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kwa kutumia nishati mbadala, ufungashaji wa vyakula vilivyosindikwa, utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali, utengenezaji wa chokaa na chaki, ukamuaji mafuta ya kula kutokana na mbegu za mafuta, utengenezaji wa sabuni na usindikaji ngozi kwa kutumia njia za asili.



Mkurugenzi Mkuu wa Sido, Profesa Sylvester Mpanduji.

"Teknolojia hizo zimesaidia kuimarisha na kuongeza ubora wa bidhaa za wajasiriamali na kuwezesha uimarishwaji wa miradi, (viwanda) 7,651 na kuanzisha viwanda vipya 4,513 vilivyotengeneza ajira 19,873," anabainisha.

Prof. Mpanduji anasema Sido pia inatekeleza ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wajasiriamali. Abainisha kuwa shirika linamiliki mitaa ya viwanda katika mikoa yote ya Tanzania Bara yenye majengo ya viwanda 467.

Anasema mitaa hiyo ya viwanda imetengwa mahususi ikiwa na miundombinu muhimu kama vile ofisi za kutolea huduma, vituo vya kuendeleza teknolojia (TDCs), vituo vya mafunzo na uzalishaji (TPCs), majengo ya viwanda, umeme, maji, barabara na mawasiliano kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati.

Prof. Mpanduji anabainisha kuwa serikali ilitoa Sh. bilioni tano mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia Sido, ili kujenga ofisi nne za kutolea huduma katika mikoa ya Simiyu, Geita na Katavi pamoja na majengo ya viwanda 12 katika mitaa ya viwanda ya Sido iliyoko Dodoma, Manyara, Kagera, Mtwara na Geita na kwamba tayari uendelezaji huo umekamilika na majengo yameanza kutumika.

Vilevile, anasema shirika linasimamia utengenezaji wa mashine na vipuri kupitia Vituo vya Maendeleo ya Teknolojia (TDCs), akibainisha kuwa linamiliki vituo vya kuendeleza teknolojia (TDCs) saba katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga.

Anasema vituo hivyo vinajihusisha na uendelezaji wa teknolojia na utengenezaji wa mashine, vifaa na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo na kati wa mjini na vijijini.

Prof. Mpanduji pia anasema shirika pia lina wajibu wa kutoa ushauri wa kiufundi kwa wajasiriamali, akibainisha kuwa limeendelea kuutoa kwa kundi hilo katika maeneo ya udhibiti wa ubora wa bidhaa, ufungaji wa mashine, ukarabati wa mashine, michoro ya majengo ya viwanda, upangaji wa mashine viwandani na uchaguzi wa teknolojia sahihi.

Anabainisha kuwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano, ushauri wa aina mbalimbali umetolewa kwa wajasiriamali 39,817 katika mikoa yote ya Tanzania Bara, huku pia wakitoa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa wajasiriamali 62,543 walioshiriki kozi 2,255.

Prof. Mpanduji pia anasema katika kipindi hicho cha miaka minne, shirika limetoa huduma za ushauri wa biashara kwa wajasiriamali wahitaji 78,574, huku likiwezesha pia upatikanaji wa masoko kwa kushirikiana na wizara kupitia kuandaa maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali wadogo ya kikanda na yale ya kitaifa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu huyo, Sido pia inawezesha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo kupitia Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF) ulioanzishwa mwaka 1994.

Anabainisha kuwa katika kipindi hicho cha miaka minne, mikopo 15,780 yenye thamani ya Sh. bilioni 35.897 ilitolewa kwa wajasiriamali. Kati yake, asilimia 53 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 47 kwa wanaume.

"Miradi iliyoanzishwa kupitia mikopo hiyo imeweza kuchangiza katika ongezeko la ajira ambapo jumla ya ajira 40,222 zimezalishwa, asilimia 53 ya ajira hizo ikiwa ni wanawake.

"Wanawake wanaonekana kunufaika na huduma hizi kwa kuwa wanaonekana kuwa na kiu zaidi ya kufanya shughuli za uzalishaji mali hasa katika maeneo ya usindikaji wa bidhaa za mazao ya kilimo na misitu," anabainisha.

Prof. Mpanduji anazitaja programu nyingine zinazotekelezwa na Sido kuwa ni pamoja na ya kongano, ambayo tangu mwaka 2006, shirika limejikita katika kuendeleza vikundi vya wajasiriamali wa viwanda vidogo ambavyo vinafanya kazi zinazofanana au kushabiiana na kuendeleza mnyororo wa thamani za bidhaa.

Anabainisha kuwa hadi mwaka 2017, jumla ya kongano 60 nchini zilianzishwa chini ya ufadhili wa wadau mbalimbali wakiwamo Sido, Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM) na LGAs.

Prof. Mpanduji anabainisha kuwa hadi sasa, Sido inafanya kazi na kongano 20. Kati yake, 18 ziko Tanzania Bara na mbili ziko Zanzibar. Anasema miongoni mwa kongano hizo, 15 zinafadhiliwa na SIDA na tano zikipata ufadhili wa JICA.

Anaitaja programu yao nyingine kuwa ni kitamizi, akifafanua: "Lengo kubwa la programu hii ni kuwawezesha na kuwasaidia wajasiriamali wabunifu katika kutekeleza mawazo yao ya ubunifu na kuyafanya kuwa halisia katika biashara zao na kusaidia ukuaji wa biashara zao na hatimaye kuzifanya biashara zao kuwa endelevu.

"Wabunifu hawa wanapata ufadhili wa majengo ya ofisi, vifaa vya kufanyia kazi zao, wanaunganishwa na taasisi mbalimbali na wanapata mikopo yenye masharti nafuu."

Mkurugenzi mkuu huyo pia anasema wana programu ya 'wilaya moja bidhaa moja', akibainisha kuwa kuanzia Julai mwaka 2007, Sido ilianzisha kaulimbiu ya Wilaya Moja Bidhaa Moja kwa lengo la kuchochea maendeleo ya viwanda vidogo wilayani.

"Mpango huu pia unalenga katika kuongea thamani ya bidhaa na kusambaza uwekezaji katika kila wilaya nchini, lakini mkakati huu unategemea upatikanaji wa rasilimali katika wilaya, mafanikio yake pia yanategemea ushiriki wa wadau, uwajibikaji katika uchambuzi, uzalishaji, usindikaji na utafutaji masoko ya bidhaa husika.

Prof. Mpanduji pia anadokeza kuwa tayari wajasiriamali wanaoendesha viwanda vyao katika mitaa ya viwanda vya Sido, wameanza kutengeneza vifaa maalum vya kunawia mikono, vitakasa mikono na mashine ya kupulizia dawa mwili mzima, ili kuisaidia nchi kukubiliana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Waziri Innocent Bashungwa, alizindua rasmi vifaa na mashine hizo hivi karibuni. Shirika linawahimiza wananchi kuwasiliana na ofisi za Sido zilipo kwenye mikoa yao ili kupata vifaa na vitakasa mikono kwa bei nafuu," anahitimisha.




Mjasiriamali Mary Muhere akiwa kwenye maonyesho ya bidhaa ya Sido mwaka jana mjini Singida. **PICHA: WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# RC aagiza walioumbuka ripoti CAG wakamatwe

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amesikitishwa na kitendo cha Halmashauri ya Manispaa ya Songea kupata hati yenye shaka na kuagiza wote waliosababisha dosari hiyo wachukuliwe hatua.

Mndeme alitoa agizo hilo wakati anazungumza kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani kilichojadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu hoja na mapendekezo yake kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Katika ripoti hiyo ya CAG, Manispaa ya Songea imepata hati yenye shaka, jambo ambalo Mndeme amesema limemsikitisha na kumuumiza.

"Ninaagiza kuanzia sasa, taratibu za kinidhamu zianze kuchukuliwa kwa wale wote waliosababisha Halmashauri ya Manispaa ya Songea kupata hati yenye shaka, hatua zichukuliwe bila kujali awe ni diwani au mtendaji. Suala hili limetutia aibu sana," aliagiza.

Mndeme aliagiza ufanyike uchunguzi ili kubaini wote waliosababisha kupatikana kwa hati hiyo kwa halmashauri hiyo ambayo alisisitiza ndiyo kioo cha Mkoa wa Ruvuma na ina kila kitu kulinganisha na halmashauri zingine za mkoa huo.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema halmashauri hiyo kupata hati yenye shaka kuwafanye madiwani na watendaji waongeze bidii na kwamba CAG ametoa hoja na mapendekezo 54, lakini yaliyojibiwa na kufungwa ni 11 tu.

Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za Serikali, Deogratias Waijaha, alitaja sababu kuu iliyosababisha halmashauri hiyo kupata hati yenye shaka kuwa ni kuripoti Sh. milioni 98 kwenye vitabu vyake vya hesabu kama mapato ya ndani ambayo majibu yake hayakupatikana.

"Ninawashauri kupitia vikao vyenu, mtafute Sh. milioni 98 kama mapato kwa sababu ile fedha itakwenda chanzo kikuu, haitarudi kwenu, lakini taratibu za kijinai ziendelee kwa wote ambao walitenda hayo makosa kulingana na sheria za nchi. Mlitakiwa kufanya mapema kabla ya kufunga hesabu," alishauri.

Waijaha alisema Manispaa ya Songea ilipata hati yenye shaka kwa tukio moja la udanganyifu wa Sh. milioni 98 na kwamba manispaa hiyo haijapata hati chafu kwa sababu vitu vingine vyote vipo sawa.

Hata hivyo, alisisitiza kuhakikisha wananunua vifaa kwa watu wenye risiti za mashine za EFD ili kuepuka kuendelea kuandikiwa hoja kutokana na kutumia watu ambao hawana risiti hizo, hali ambayo inaikosesha serikali mapato.

Meya wa Manispaa ya Songea, Alhaj Abdul Hassan Mshaweji, kwa niaba ya madiwani na watendaji, aliahidi kufanyia kazi mara moja maagizo yote ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na CAG.

NMB
Karibu yako

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 20 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 20 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika kwa njia ya mtandao saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 5, 2020. Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

20.1 MATANGAZO NA AKIDI

20.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

20.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 19 ULIOFANYIKA TAREHE 15 JUNI 2019

20.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 19 WA WANAHISA

20.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2019

20.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2019

20.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

20.8 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI

20.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI

20.10 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2020

20.11 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima atume kwa njia ya mtandao nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni (kwa njia ya mkono au mtandao) kabla ya saa 4 asubuhi Ijumaa ya tarehe 4 Juni 2020.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya NMB (www.nmbbank.co.tz).
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 96 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 48 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2019.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **15 Mei 2020** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **15 Mei 2020** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **4 Juni 2020** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **5 Juni 2020 nakuendelea** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **9 Juni 2020** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa:** | **kuanzia tarehe 17 Juni 2020** |

Lilian R. Komwihangiro
**Katibu wa Kampuni**

8 Mei 2020

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF isitwishwe zigo la vibanda umiza

**BAADA** ya kimya cha takriban mwezi mmoja na wiki tatu sasa, hatimaye Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imeweka wazi endapo itapata baraka za serikali inatarajia kuruhusu ligi za soka nchini kurejea mapema Juni mwaka huu.

Hatua hiyo ya TPLB imekuja baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kueleza anafikiria kwa siku zijazo kuruhusu ligi za soka kuendelea na anachosubiri ni kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wake.

Kauli hiyo ya Rais Magufuli ilikuja wakati muafaka ambapo TPLB na Shirikisho la Soka nchini lilikuwa katika kikao cha pamoja kujadili hatima ya Ligi Kuu kufuatia agizo la Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

Hiyo ni baada ya mwishoni mwa Aprili Caf kuwataka wanachama wake, ikiwamo TFF hadi ifikapo Mei 5, kila shirikisho kueleza hatima ya ligi yake endapo itaendelea ama kufutwa ili iweze kupanga kalenda yake ya michuano mbalimbali.

Caf ililazimika kutoa kauli hiyo kutokana na karibu ligi zote barani Afrika kusimama kwa kipindi kisichojulikana baada ya mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19), ambavyo hadi jana mchana jumla ya watu 4,114,896 duniani kote walishabainika kupatwa na maambukizo huku waliopona wakiwa 1,445,980 na waliopoteza maisha wakiwa 280,564.

Kwa Tanzania pekee maambukizo yamefikia 509, vifo vikiwa 21 na waliopona wakiwa 183, idadi hiyo ikiwa ni ongezeka la watu 508 kutoka mtu mmoja aliyekuwa na maambukizo wakati serikali inatangaza kusitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo Machi 17, mwaka huu.

Tayari TFF imeeleza kuwa wakati ikisubiri baraka za serikali ya ruhusa ya ligi hiyo kurejea, mbali na tahadhari zote kufuatwa kama inavyoelekezwa na wizara ya afya, pia huenda wakaruhusu mashabiki wachache mno kuingia viwanjani ama kuwazuia kabisa.

Hata hivyo, kumeibuka mjadala mzito kutoka kwa wadau wa soka wakihoji namna TFF itakavyoweza kuzuia mashabiki wanaokusanyika katika kumbi mbalimbali za starehe, baa na vibanda umiza kushuhudia mechi.

Wengi wanadai ni rahisi kwa TFF kuzuia mashabiki kuingia viwanjani wakati wa mechi, lakini ni kazi kubwa kwa shirikisho hilo kuweza kuzuia watu kukusanyika katika vibanda umiza na kumbi za starehe kuangalia mechi jambo ambalo wanaona kuruhusiwa kurejea kwa ligi hiyo kutazidisha maambukizo.

Kwanza kabisa kama ambavyo katika nyakati tofauti Rais Magufuli amenukuliwa akisema Watanzania waendelee kuchapa kazi na kuchukua tahadhari zote kama inavyoelekezwa na wizara ya afya, tunaunga mkono kauli hiyo.

Pia tukumbuke Ujerumani ambapo kuna jumla ya watu 171,324 waliopatwa na maambukizo huku vifo vikiwa 7,549 na walipona kati yao wakiwa 144,400, idadi ambayo ni zaidi ya Tanzania, lakini serikali ya nchini humo imeruhusu Ligi Kuu ya Bundesliga kuendelea na inatarajiwa kurejea rasmi Jumamosi wiki hii kwa tahadhari zote kuchukuliwa, hivyo hili la kuhofia mashabiki kurundikana katika vibanda umiza lisiwe sababu ya kuzuia ligi kurejea.


Na katika hilo, jukumu la TFF liendelee kubaki kuhakikisha tahadhari zote zinachukuliwa endapo wataruhusu mashabiki wachache kuingia viwanjani ikiwa ni pamoja na kulinda afya za wachezaji, lakini hili la vibanda umiza na baa linapaswa kuwa la kila mmoja kuchukua tahadhari.

Tunasema hilo kwa kuamini kuwa elimu ambayo imeshatolewa na inayoendelea kutolewa kila uchao kuhusu namna ya kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona imewafikia wengi na ni wakati sasa wa kuchapa kazi na kuendelea kuchukua tahadhari.

Hivyo, shughuli za kiserikali, uzalishaji mali ikiwamo michezo na maisha ya kila siku lazima yaendelee huku kila mmoja akichukua tahadhari ya kujikinga na janga hili la dunia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vituo vya TV za kurusha mechi viongezwe kupunguza corona

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya sasa kuwapo kwa uwezekano wa Ligi Kuu Tanzania Bara kuendelea na kuumalizia msimu wa 2019/20 ambao umekumbwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa COVID-19, maarufu kama corona, kumekuwa na mipango na mikakati mbalimbali ili kuona inamalizika kwa usalama na amani.

Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) imesema huenda ligi ikarejea tena Juni mwaka huu, lakini ikichezwa kwa mtindo ule ule wa nyumbani na ugenini, ingawa baadhi ya klabu zimeonyesha kupinga kutokana na kudai kukabiliwa na ukata, lakini mechi zilizosalia kwa kiasi kikubwa zitachezwa bila mashabiki uwanjani.

Na hii ni kutokana na kwamba pamoja na ligi inarejea, bado janga hilo lipo, lakini maisha ni lazima yaendelee na watu waendelee kuchapa kazi.

Hebu fikiria, wakati ule mashabiki wanaruhusiwa tu kwenda viwanjani, lakini kwenye vibanda umiza watu wanajazana kuangalia mechi mbalimbali za ligi, je, wakati huu ambako haruhusiwi shabiki yeyote kuingia uwanjani, zaidi ya wachezaji, viongozi, makocha, madaktari, wahudumu, walinzi na askari tu?

Ni kwamba wale mashabiki wote waliokuwa na tabia za kwenda viwanjani, sasa nao wataongeza idadi ya wale watakaojazana kwenye vibanda umiza.

Si huko tu, hata kwenye hoteli na baa mbalimbali, zitakuwa na shughuli kubwa ya kupokea wateja wengi wanaokwenda kutazama mechi.

Hii itasababisha watu wengi kuwa kwenye hatari zaidi ya kuambukizwa corona kwenye maeneo ya msongamano wa watu wanaoangalia mpira.

Tukumbuke kuwa waangaliaji mpira si sawa na watu waliokusanyika kwenye mikusanyiko mingine, mara nyingi muda mwingi wanaongea, wanabishana, wanapigana vijembe, wanashikana na kushangilia kwa nguvu, wakirukaruka, hivyo ni watu ambao wako kwenye hatari zaidi.

Kwa hali hiyo, itakuwa ni kazi bure kuwakataza watu wasiingie uwanjani, lakini wanaachwa kwenye maeneo mengine wakusanyike.

Hata hivyo, ni televisheni moja tu ndiyo iliyoingia mkataba wa kuonyesha mechi hizo, ambapo wafanyabiashara hununua ving'amuzi vyao kwa ajili ya kuonyesha mechi za Ligi Kuu.

Sina tatizo na hilo kwa sababu ni kweli wana haki kisheria, lakini kwa maoni yangu ni kwamba kutokana na janga hili kila kitu kinaweza kubadilika kwa kipindi hiki ili tu kulinda afya za watu na kuwafanya waendelee kujenga taifa, kufanya kazi na kulipa kodi.

Mimi nadhani kwa kipindi hiki, kwa mechi zilizobaki, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na kampuni ya Televisheni ya Azam iliyonunua haki za kurusha mechi za Ligi Kuu wakae chini na kuzungumza ikiwezekana kuuza haki hiyo kwa vituo vingi zaidi vya televisheni kwa makubaliano maalum ya kibiashara ili nazo zijiunge nayo kwa ajili ya kuonyesha mechi hizo, hatua ambayo itapunguza msongamano wa mashabiki kwenye maeneo zinapoonyeshwa mechi.

Tumeshawahi kuona huko nyuma kwenye sherehe za kitaifa, Rais akihutubia, au misiba ya watu mbalimbali mashuhuri, televisheni zote zimeungana na televisheni moja tu kwa ajili ya kuonyesha tukio hilo.

Kwa hili pia inawezekana kufanyika hivyo lengo likiwa ni moja tu, kuepusha msongamano kwenye maeneo mbalimbali ya kuonyesha soka.

Wigo unapokuwa mpana, na televisheni kadhaa ikiwamo hata ya taifa, zikijitokeza kuonyesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobaki, basi hakutokuwa na misongamano mikubwa kwa sababu wengine watabaki wakiangalia majumbani mwao.

Najua kuna baadhi ya mashabiki wao hawawezi kuangalia nyumbani kwa sababu kuna utulivu, badala yake wanataka sehemu za kubishana, lakini kwa kiasi kikubwa kutakuwa hakuna misongamano na hata wamiliki wanaweza kumudu kuchukua hatua za kuwanawisha kwa sabuni na dawa, kuliko umati mkubwa ukijazana.

Wakati mwingine watu wanajazana sana kwenye vibanda umiza kwa sababu ya uchache wa maeneo ya kuonyesha mpira, hivyo televisheni kubwa nchini Tanzania zikionyesha itapunguza msongamano mabandani.

Nadhani Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, ikishiriakiana na TFF, TPLB na Azam TV yenye haki ya kuonyesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, wanaweza kukaa na kuliweka sawa hili ili mechi ziendelee kuchezwa na kuonwa kwa mapana zaidi huku afya za Watanzania zikiwa zimezingatiwa.

# Ushetu wakabidhiwa gari kubeba wagonjwa

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

WANANCHI wa Halmashauri ya Ushetu wamekabidhiwa gari la kubeba wagonjwa lenye thamani ya Sh. milioni 120, lililotolewa na Wizara ya Afya kwa ufadhili wa Global Fund.

Gari hilo ambalo ni sehemu ya mkakati wa serikali kupunguza vifo vya watoto, wajawazito na wagonjwa wa kawaida wenye uhitaji wa rufani, lilikabidhiwa kwa wananchi mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Ushetu, Elias Kwandikwa.

Naibu Waziri huyo wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, akiwa ameambatana na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Azzah Hilal, alikabidhi gari hilo kwenye Kituo cha Afya Mbika pamoja vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona vyenye thamani ya Sh. milioni moja.

Kwandikwa alisema kuwa gari hilo lililotolewa na Wizara ya Afya, lina thamani ya Sh. milioni 120 na ilipendekezwa liwekwe kwenye kituo hicho kwa kuwa kinahudumia idadi kubwa ya wagonjwa, baadhi yao wakitoka mkoa jirani wa Tabora.

"Gari hili ni maalum kwa kubeba wagonjwa wenye uhitaji wa rufani, mama wajawazito na watoto, limetolewa na Wizara ya Afya na mimi nikapewa kuja kulikabidhi katika kituo hiki.

"Ninafahamu vituo vipo vingi havina magari, pale penye ulazima vituo vingine wanaweza kuja kuazima kwa dharura na kuweka mafuta," alifafanua.

Azzah kwa upande wake, alisema kutokana na matatizo yanayowapata wajawazito na watoto na kusababisha kupoteza maisha kutokana na kutopata rufani za matibabu kwa wakati, wadau wa afya wameona watoe gari hilo.

Alisema kutolewa kwa gari hilo kumetokana na ombi lake kwa Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, alipokuwa ziarani mkoani Shinyanga, akikumbusha kuwa alimwomba kuwasaidia kutatua tatizo la ukosefu wa usafiri kwa ajili ya wagonjwa na sasa serikali imetekeleza.

"Ndani ya miaka mitano, yamekuwapo mabadiliko katika sekta ya afya kwa kuboresha vituo vya afya na vingine kuongezeka. Hata Jimbo la Ushetu tumeboresha vituo vya afya, mfano Kituo cha Afya Ukune mwaka 2018, nilimwomba Waziri Mkuu gari la kubebea wagonjwa na sasa tumelipata," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu, Juma Kimisha, alisema halmashauri hiyo ina kata 20 na ina vituo vya afya vitatu na zahanati 22 vinavyomilikiwa na serikali na vile vya binafsi viko saba.

Alisema halmashauri hiyo kijiografia eneo lake linategemewa kwa huduma za afya na wananchi wanaotoka Urambo ambao wanapata matibabu kwenye Kituo cha Afya Mbika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomora, aliwataka watumishi wa Kituo cha Afya Mbika kulitunza gari hilo na litumike kwa mambo yaliyokusudiwa tu.

Diwani wa Ushetu, Pili Sonje, alieleza kufurahishwa na hatua hiyo ya serikali kukabidhi gari hilo, akibainisha kuwa walikuwa wanapata shida kuwasafirisha wagonjwa kwa kukodi pikipiki na magari kwa gharama kubwa kwenda mjini Kahama kupata matibabu ya magonjwa ambayo yalishindikana kupatiwa ufumbuzi katika kituo hicho.



Maofisa wa Jeshi la Polisi Morogoro wakisimamia kazi ya kuhesabu sarafu za Sh. 200 zenye thamani ya Sh. milioni 200, mali ya kampuni ya michezo ya kubashiri ya Bonanza zilizokamatwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, baada ya kubainika kuhifadhiwa kwenye nyumba kinyume cha sheria. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Kaya maskini zasaidiwa vyakula, vifaa vya corona

**Na Beatrice Philemon**

SHIRIKA la Kimataifa la Holt Children's Services Incorporation la Korea Kusini kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Women In Social Entrepreneurship (WISE), wametoa msaada wa vyakula, barakoa na sabuni vyenye thamani ya Sh. milioni tano kwa kaya maskini 109 katika Kata ya Keko Mwanga B, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Meneja mradi wa Holt Children Service, Vaileth Loy, alisema jumla ya mifuko 109 ya unga wa mahindi, barakoa 545 na miche ya sabuni 327 ilitolewa kwa kaya hizo, na kila kaya ilipata kilo 25 za unga wa mahindi, barakoa tano na miche mitatu ya sabuni.

Alisema wameamua kutoa msaada huo ili kuzipa ahueni kaya maskini hasa katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona, ambapo wanaangaika kupata chakula na kuwasaidia kupambana na maambukizo ya virusi vya corona.

"Kwa niaba ya walengwa wetu, tunalishukuru Shirika la Holt Children Service Incorporation na watu wa Korea Kusini kwa ukarimu wao kwa wananchi hawa katika kipindi hiki cha uhitaji mkubwa wa kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa corona, kwa sababu kaya nyingi katika eneo hili zina hali mbaya, na wengi wameathirika kwa njaa tangu ugonjwa wa corona uingie nchini," alisema.

Alisema kutokana na corona, wengi waliojikita katika sekta isiyo rasmi wameathirika zaidi ikiwamo kupungua au kupoteza kipato kabisa na kusababisha kuongezeka ukali wa maisha.

Pia alisema watoto wao kuendelea kuwapo nyumbani kutokana na shule kufungwa, kumechangia kwa kiasi kikubwa fedha zao za biashara kushindwa kuzunguka, na kukwama kufanya biashara.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Holt Children's Services Incorporation, Jeun Park, alisema wameamua kutoa msaada huo baada ya kuona wakazi wengi wa Keko Mwanga 'B' wana hali mbaya, wanaishi katika mazingira magumu na wanaangaika kupata chakula kwa ajili ya kulisha familia zao.

"Wazazi wengi wamekuwa na hali mbaya katika kipindi hiki kwa sababu kinamama wengi hawaendi kazini, fedha nyingi walizokuwa wakipata katika biashara zao ndogo ndogo sasa zinatumika kununua chakula kwa ajili ya familia na matokeo yake wanashindwa kuendeleza biashara zao na hali inazidi kuwa mbaya," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wise, Dk. Astronaut Bagile, aliwaomba wadau nchini kuangalia kaya zinazoishi kwenye mazingira magumu na wafikirie jinsi gani wanaweza kujikinga na corona.

# Madiwani wataka ushiriki Wahadzabe tiba ya virusi corona

**Na Elisante John, SINGIDA**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetakiwa kupeleka wataalamu wake mkoani Singida, kutafuta uwezekano wa kupata tiba ya ugonjwa wa COVID-19 kwa jamii ya Wahadzabe, inayoishi pori la Kipamba, Wilaya ya Mkalama.

Wakizungumza kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, ilielezwa kuwa kutokana na kukosekana kwa dawa ya kutibu COVID-19, ni vyema jamii ya Kihadzabe ikashirikishwa kwa dhati kupata tiba ya gonjwa hilo.

Ombi hilo lilitolewa na madiwani mwishoni mwa wiki kupitia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega.

"Kutokana na janga hili kuenea nchini na dunia kwa ujumla, ni vizuri wataalamu kutoka Wizara ya Afya, waje Mkalama wakutane na jamii yetu ya Kihadzabe inayotegemea tiba ya asili ili washirikiane kupata dawa au kinga ya kutibu virusi vya corona," alisema Mkwega.

Naye Diwani Eunic Kalaila, aliunga mkono hoja hiyo kwa kukitaka kitengo cha tiba wizarani, kufanya kazi hiyo, hasa wakati huu ambao serikali imeitambua jamii hiyo, tofauti na miaka ya nyuma.

Alisema jamii ya Kihadzabe ikishirikishwa kwa dhati na timu ya wataalamu wa afya kutoka wizarani, anao uhakika wa kupatikana kwa tiba ya COVID-19, unaoitesa dunia hivi sasa.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Matongo, John Linza na Silvester Marmo wa Kata ya Kinampundu, waliunga mkono kauli hiyo ili jamii ya Wahadzabe iongeze nguvu katika mapambano dhidi ya virusi hatari vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

"Jamii ya Wahadzabe inatumia dawa za asili na hata sasa wapo porini, na wakiugua wao hawaendi kutibiwa hospitalini kupewa hizi dawa zetu kutoka kwa wataalamu, wao huchimba mizizi ya miti wanayoijua wao na kutibu, halafu wanapona," alisema Marmo.

# 'Wanaomechisha' uvaaji barakoa wamkera DC

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, amesema anachukizwa na baadhi ya wananchi wanaojaribisha barakoa na kurejesha wakati wa ununuzi na wanaovaa barakoa zinazofanana na mavazi yao.

Kiongozi huyo wa wilaya pia amewataka wananchi kutambua kwamba, siyo kila kifo kinachotokea wilayani mwake kinasababishwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Macha aliyasema hayo jana alipopokea msaada wa chakula na vitakasa mikono kwa ajili ya wananchi waliokumbwa na maafa katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini kutoka Shirika la Msalaba Mwekundu Kahama.

Alisema kuwa, mbele ya geti la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, wananchi wanachagua barakoa kwa kuzijaribisha na kuzirejesha kwa muuzaji, huku wengine wakichagua rangi ambazo zinaendana na mavazi yao badala ya kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

"Ninakerwa na baadhi ya wananchi hasa wanawake wanaonunua barakoa kwa kuzijaribisha kama zinawatosha na kuendana na mavazi wanayokuwa wamevaa. Tunaleta mzaha kwenye kupambana na Covid-19 na huku tunatambua ni hatari sana," alisema.

"Pia, lazima tutambue kwamba siyo kila kifo kinachokea hapa, kinatokana na ugonjwa wa corona, vifo vingine vinatokea kwa kusababishwa na malaria, Ukimwi pamoja na mapafu kutofanya kazi vema, hivyo tusihisi vifo vinavyotokea ni corona tu," aliongeza.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Lucas Devidi, alisema wameshawaondoa wajasiriamali waliokuwa wanauza barakoa za vitambaa mbele ya geti la hospitali hiyo.

Akikabidhi msaada wa chakula na vitakasa mikono, Mratibu na Hamasa Msalaba Mwekundu Kahama, Anna Martini, alisema wamekabidhi mchele kilo 86, unga kilo 90, sabuni miche minne, sanitizer lita 10 na dagaa visado vinne.



Ofisa Utawala wa kampuni ya Vilipuzi ya African Exploration Tanzania Ltd, Asnat Ibrahim (wapili kulia), akikabidhi barakoa kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva wa Tegeta na Bunju (Uwawate), Mohamed Mselem, kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona zilizotolewa na kampuni hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaingilia kati mikopo ya kinyonyaji kwa watumishi

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

UONGOZI wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, umeamua kuingilia kati mgogoro uliopo kati ya watumishi wa umma na wakopeshaji binafsi ambao wamekuwa wakiwadai watumishi madeni yenye riba kubwa.

Katika kushughulikia suala hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Said Mtanda, aliitisha kikao kilichohudhuriwa na walimu 79 na wakopeshaji binafsi kwa lengo la kutafuta suluhu.

Katika kikao hicho ilibainika kuwa riba inayotozwa na wakopeshaji hao ni kubwa na kinyume cha sheria zinazoielekeza taasisi za fedha kiwango cha utozaji riba, hali inayosababisha watumishi wengi hasa walimu kuamua kujificha na kutoonekana mitaani kutokana na kuwaogopa wakopeshaji hao.

Mmoja wa walimu hao, Halji Kumbakumba, alisema alikopa Sh. milioni 4.7 na sasa analazimika kulipa Sh. milioni 10 kama riba ya mkopo huo na anaona riba za wakopeshaji hao ni uonevu unaowafanya wakopaji kuishi maisha magumu.

Agnes Mwanisawa, mtumishi mwingine katika halmashauri hiyo, alisema alidai alikopa Sh. 110,000 na alitakiwa kulipa Sh. 160,000 na tayari ameshalipa Sh. 150,000, lakini kutokana na kuchelewa kwa mwezi mmoja kurejesha Sh. 10,000 iliyobaki, anatakiwa kulipa Sh. 110,000 kama riba ya Sh. 10,000.

Kutokana na hali hiyo, Mtanda aliwagiza Kaimu Ofisa Elimu (shule za msingi) wilayani Nkasi, Jesca Lwiza, kuandaa mikataba kulingana na fedha wanazodaiwa walimu hao na kuwataka walimu wote na wakopeshaji binafsi kufika ofisini kwake Jumatatu (leo) kutia saini mikataba halali ya fedha wanazodaiwa na muda wa kulipa na kusisitiza riba za kinyonyaji hazitakubalika.

Alisema lengo lake ni kutafuta suluhu ya tatizo hilo, akiahidi pia kuwasiliana na Benki Kuu (BoT) Kanda ya Mbeya ili kujiridhisha kama wakopeshaji hao wana vibali halali vya kufanya kazi hiyo na kujua riba halali iliyowekwa na serikali kwa taasisi za fedha za mikopo.

Mkuu wa Wilaya huyo pia aliwataka walimu kuacha kwenda kukopa fedha kwa wakopeshaji binafsi ili kuepuka migogoro na unyoanyaji kupitia mikopo.

# H/shauri zapewa somo mapato zaidi ya ndani

**Na Tiganya Vincent, URAMBO**

HALMASHAURI ambazo zinazotegemea sehemu ya mapato kutoka kwenye zao la tumbaku, zimetakiwa kuandaa mkakati mpya ambao utawawezesha kulima mazao mengine ili kuwa na vyanzo vipya vya mapato ya ndani.

Hatua hiyo inafuatia kampuni zinazonunua tumbaku mkoani Tabora kuendelea kushusha makisio ya uzalishaji kwa wakulima wa tumbaku.

Ushauri huo ulitolewa jana na Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Urambo.

Alisema Kampuni za Tumbaku zimekuja na staili mpya ya kudai kuwa zitanunua tumbaku kilo chache, badala yake zimekuwa zikinunua tumbaku nyingi iliyolimwa nje ya mkataba kwa bei inayomuumiza mkulima na kusababisha halmashauri kupata mapato kidogo.

Aidha, Makungu alisema ni vema halmashauri zikaanzisha kilimo kikubwa cha maembe kwa kuwa mfanyabiashara Bakharesa ameshaonyesha nia ya kununua embe zote zinazozalishwa mkoani Tabora.

Alisema cha msingi kuwaelimisha wakulima kulima kitaalamu na kutoa huduma za ugani kwao ili waweze kuzalisha maembe bora.

Makungu aliongeza ni vema halmashauri zikasisitiza kilimo cha korosho na alizeti kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kuwa na vyanzo vingi vya kujipatia kipato.

Wakati huo huo, Mkoa wa Tabora umeagiza kuchukuliwa hatua za kisheria dhidi ya watumishi wote waliopewa mashine za kukusanyia mapato (POS) ambao wanadaiwa mapato waliyokusanya kutoyawasilisha benki.

Agizo hilo lilitolewa na Makungu wakati wa kikao hicho, na kueleza kuwa kitendo hicho ni kinyume cha kifungu cha 60 cha Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001.

Makungu alisema dosari za aina hiyo ndio zimekuwa zikisababisha upotevu wa fedha za umma, na kuziagiza halmashauri kuhakikisha zinasimamia kwa ajili ya kuziondoa.

HABARI KITAIFA

# Askari wanyamapori wakwaa kashfa nzito

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MBUNGE wa Kondoa Mjini (CCM), Edwin Sannda, ameibua kashfa bungeni akiwatuhumu baadhi ya askari wa Pori la Akiba la Swagaswaga, kuwashambulia kwa risasi wafugaji kisha kupora mifugo yao.

Vilevile, amedai askari hao kumdhulumu mifugo bibi wa miaka 60 na kumwomba rushwa ya Sh. milioni 1.5, akiitaka serikali kuwachukulia hatua kali watumishi hao.

Akichangia hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Malisili na Utalii bungeni jijini hapa, Sannda alisema liko tatizo kubwa la kukosa uadilifu na weledi kwa baadhi ya askari wa wanyamapori na baadhi ya watumishi wa wizara kuonekana kubariki hujuma na dhuluma dhidi ya wafugaji kwa kivuli cha kusimamia sheria za uhifadhi.

"Askari wanakwenda vijijini wanapiga silaha za moto hewani, mifugo inakimbilia porini, wanakwenda wanawakamata, wanaanza kunyanyasa wananchi, wanawapiga, wanawatesa kabisa kwa adhabu kinyume kabisa na haki za binadamu, wanadai rushwa na wanauza ile mifugo, wanachinja," alilalamika.

Mbunge huyo alisema anayo kesi mahususi ya dhuluma na uonevu dhidi ya wananchi ambapo mwaka jana kijana mmoja mifugo yake 145 ilikamatwa na baada ya kesi kuendeshwa, imekuja kubainika hana hatia na hakuwa na kosa na kutakiwa arejeshewe mifugo yake, lakini jambo la kusikitisha kati ya mifugo 145 iliyokamatwa, ni 33 tu iliyorudishwa.

"Yuko bibi tena wa miaka 60, amekamatiwa mifugo yake 22 kimakosa, baadaye inaamriwa arejeshewe mifugo yake, amerudishiwa mitatu tu halafu wanamwomba bibi yule rushwa ya Sh. milioni 1.5," alisema.

Mbunge huyo alisema tayari malalamiko hayo ya wafugaji alishayafikisha kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Wanyamapori (Tawa) na tayari amepeleka kamati kwa ajili uchunguzi dhidi ya tuhuma hizo.

Mbunge huyo alitaka kuwapo mfumo mzuri wa kufanya uchunguzi na kufanya ufuatiliaji wa haraka pindi kunapotokea matukio ya aina hiyo ambayo yakiachwa yaendelee yanaichafua serikali mbele ya wananchi. Mbunge huyo alisema manyanyaso na dhuluma dhidi ya wafugaji hayako kwenye Pori la Swagaswaga, bali katika maeneo yote nchini lakini jambo la kusikitisha, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na wizara kudhibiti uovu huo.

Mbali na manyanyaso dhidi ya wafugaji pia mbunge huyo alielezea kutoridhiwa na utaratibu wa malipo ya vifuta jasho pamoja na vifuta machozi kwa kuwa umekuwa ukichukua muda mrefu na wakati mwingine anakuja kulipwa mtu wa miaka ya mbele anaachwa yule wa miaka ya nyuma au anasahauliwa.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alikiri kuchelewa kulipwa kwa baadhi ya wananchi, lakini hadi sasa tayari wameshalipa Sh. bilioni moja kama kifuta machozi katika maeneo mbalimbali nchini na kuna madai ya kifuta machozi ya Sh. bilioni 2.2 ambayo yako kwenye hatua za kulipwa.

"Ucheleweshaji wa madai unatokana na kuchelewa kupokea madai kutoka wilaya husika, zilikuwa zinachelewa kufika lakini sasa tumeteua ofisa wa kusimamia suala hili ili kuondoa tatizo la ucheleweshaji malipo," Kanyasu alisema na kuahidi kufuatilia malalamiko mengine ya mbunge huyo.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), Prof Costa Mahalu (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Real PR Solutions (RPR), Kanda ya Ziwa, Magreth Laizer (kushoto), wakisaini makubaliano ya utekelezaji wa pamoja mpango wa mafunzo kwa wadau wa utalii, unaolenga kutoa mafunzo kuhusu namna bora ya kuendesha, kukuza na kutambua fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Programu mafunzo fursa za utalii yaja

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

PROGRAMU ya mafunzo ya kuhusu namna bora ya kuendesha, kukuza na kutambua fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii nchini inatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni jijini Mwanza.

Zaidi, mafunzo hayo yanalenga pia kuandaa wadau wa utalii nchini ili waweze kutoa huduma zao kwa weledi huku wakizingatia kanuni za kiafya pindi sekta hiyo itakapoimarika baada ya kuathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na janga la ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) unaosababishwa na virus vya corona ambalo limeyakumba mataifa mengi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini Mwanza wakati wa hafla fupi ya kusaini hati ya makubaliano kuhusu utekelezaji wa programu hiyo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), Prof. Costa Mahalu, alisema programu hiyo itatekelezwa kwa ushirikiano wa karibu baina ya chuo hicho pamoja na Kampuni ya Real Pr Solutions (RPR).

Kulingana na makubaliano hayo, SAUT itahusika katika utoaji wa mafunzo hayo yanayotarajiwa kuanza mwishoni mwa Juni mwaka huu, sambamba na kutoa vyeti kwa wahitimu huku kampuni ya RPR ikihusika katika kutafuta fedha za uwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka kwa wadau mbalimbali hususani mashirika na taasisi zinazohusika na sekta hiyo.

"Mlipuko wa COVID-19 ni kama umesababisha dunia isimame kwa muda kwa maana kuwa mataifa mengi hususani yale tunayoyategemea kwenye masuala ya utalii yamewafungia raia wake ndani na huduma za ndege pia zimefungwa. Hali hiyo imesababisha athari kubwa kiuchumi hususani katika sekta ya utalii hapa nchini kama ambavyo waziri anayehusika na utalii nchini alivyobainisha hivi karibuni. SAUT na wadau wengine tumechukua hatua na mafunzo haya kwa wadau wa utalii utasaidia kuiboresha tena sekta hii muhimu," alisema Prof. Mahalu.

Alisema SAUT na RPR zinafanya kazi kwa mashauriano ya karibu na washirika wengine ili kusaidia sekta ya utalii na kuhakikisha sekta hiyo inarejea kikamilifu, huku pia wadau wakichukua tahadhari zote za kiafya dhidi ya virusi vya corona. Aliongeza kwamba mpango pia unalenga kuwaandaa vizuri wakazi wa Kanda ya Ziwa ili wawe mstari wa mbele kuunadi utalii uliopo kanda hiyo.

"Tunatarajia kwamba awamu ya kwanza ya programu yetu itaanza na Jiji la Mwanza ambapo tunalenga kuwafikia wadau wengi iwezekanavyo watakaotoka wilaya zote za mkoa wa Mwanza ambapo tumejipanga kupokea watu wasiopungua 2000 watakaopata mafunzo kwa awamu, alisema, huku akiitaja mikoa itakayofuata kuwa itakuwa ni Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara na Kagera.

# Shehena vipodozi visivyoruhusiwa nchini vya mamilioni yakamatwa

**Na Manuel Kaminyoge, SONGWE**

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe limekamata shehena ya vipodozi vyenye viambata vya sumu maboksi 196 vilivyopigwa marufuku kuingia nchini.

Vipodozi hivyo vilikuwa vikiingizwa kwa njia ya magendo vikiwa na thamani ya Sh. milioni 98.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alisema vipodozi hivyo vilikamatwa katika doria iliyofanyika usiku vikiwa kwenye gari T910 ABN aina ya Mitsubishi Canter ikitokea nchini Zambia na kuingia Tanzania kwa magendo.

Kamanda Kyando alisema kuwa ni matukio ya mwendelezo kwa shehena za vipodozi kukamatwa katika mpaka wa Tanzania na Zambia.

Kamanda Kyando alisema juzi usiku katika maeneo ya mtaa wa Kichangani kata ya Chapwa, tarafa ya Tunduma wilaya ya Momba, polisi wakiwa katika msako kwa kushirikiana na vyombo vingine za ulinzi na usalama, walikamata vipodozi aina mbalimbali katoni 199 ambavyo vimepigwa marufuku kuingia nchini.

Alisema mmiliki wa gari hajajitokeza na dereva aliyekuwa analiendesha alikimbia na kuwataka kujisalimishe.

# Waziri atoa siku 10 ripoti athari bwawa la Kidatu

**Na Mwandishi Wetu, KIDATU**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, amewapa siku kumi wataalamu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Tanesco na wadau wengine kufanya utafiti na kutoa ripoti ya tathmini ya athari kwa mazingira kufuatia kuongezeka kwa maji kupita kiasi katika mabwawa ya kufua umeme.

Waziri Zungu aliyasema hayo alipofanya ziara ya pamoja na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, iliyolenga kujionea hali ya bwawa la Kidatu ilivyo kufuatia kujaa maji kupita kiasi, jambo lililosababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo baada ya kurudi maji hayo kupita.

"Muhimu kufanya utafit juu ya athari zilizojitokeza kutokana na kuongezeka kwa maji kwenye mabwawa ikiwa ni pamoja na kupima kiwango cha matope," alisema Waziri Zungu.

Waziri Zungu alisema inawezekana mabwawa yakawa yamejaa matope kwa chini, hivyo suala la kuyafungulia maji ili kuepuka kutokea tatizo la kushindwa kuzalisha umeme kwa kiwango kinachotakiwa.

"Mradi wa umeme Mto Rufiji unategemea uwapo wa maji ya kutosha kutoka katika vyanzo hivyo vya maji na kuna kila sababu ya kufanya utafiti ili kivilinda vyanzo hivyo ili maji yakalijaze bwawa hilo," alisema Waziri Zungu.

Alisema wizara yake ndiyo yenye dhamana na mazingira, hivyo itahakikisha mazingira katika vyanzo vyote vya maji vinalindwa na kuhifadhiwa ili kuwa na uhakika wa maji ya kuendesha uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Mto Rufiji.

"Serikali imewekeza fedha nyingi kuhakikisha ujenzi wa mradi wa umeme Mto Rufiji unakamilika, hivyo ni jukumu letu sasa kufanya mradi huu unakuwa endelevu kwa kutunza vyanzo vya maji," alisema Zungu.

Alisema elimu kwa wananchi iendelee kutolewa hususani ya kufanya shughuli za kiuchumi kando au pembezoni mwa mito na vyanzo vya maji ili kutoathiri upatikanaji wa maji kwenye mabwawa yanayozalisha umeme.

Kwa upande wake, Dk. Kalemani alisema wizara yake ilishaunda kamati ya kufanya tathmini hiyo ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa na maji yanayopatikana yakawezeshe bwawa kubwa la Mto Rufiji kupata maji kwa ajili ya kuzalisha umeme wa megawati 2,115.

"Maji yanayohitajika katika bwawa la Rufiji ni zaidi ya mita za ujazo bilioni 32, hivyo ni muhimu vyanzo vya maji vilindwe kikamilifu," alisema Waziri Kalemani.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Sanare, alisema mkoa umeshaanza kutoa elimu kwa wananchi na kuwataka wote waliojenga kando ya mto kuhama ili kuepukana na majanga ya mafuriko.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka alisema baraza limepokea maelekezo ya waziri na tayari timu ya wataalamu ipo kazini kuhakikisha ripoti ya tathmini ya mazingira inakamilika katika muda uliopangwa.

## Ujenzi jengo la kinamama Sekou Toure wafikia 50%

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

UJENZI wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure), umefikia asilimia 50 na utakapokamilika utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 10.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Bahati Msaki, ndiye aliyebainisha hayo alipozungumza na Nipashe na kufafanua kwamba ukikamilika utasaidia kuondoa mrundikano wa wagonjwa wodini kwa wajawazito wanaosubiri kujifungua pamoja na watoto.

Dk. Msaki alisema kuwa ujenzi huo pia utasaidia kuondoa changamoto ya ufinyu wa chumba cha upasuaji kwa wagonjwa, ambao unatarajiwa kukamilika mapema mwaka huu.

Aidha, jengo hilo litakuwa na huduma za kliniki ya wajawazito na watoto, duka la dawa pamoja na maabara.

Aliishukuru serikali kwa kuwapatia fedha hizo kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika hospitali hiyo.

**Dk. Msaki alisema kuwa ujenzi huo pia utasaidia kuondoa changamoto ya ufinyu wa chumba cha upasuaji kwa wagonjwa, ambao unatarajiwa kukamilika mapema mwaka huu.**



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (kushoto), akizungumza na mmoja wa mwenye nyumba katika kijiji cha Kwasunga, wilayani Korogwe mkoani Tanga, baada ya kuwasha umeme katika nyumba hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC afuatilia utekelezaji maagizo ya JPM

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

VIONGOZI wa Serikali Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, wametakiwa kukamilisha haraka ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Magubike, katika tarafa ya Magole ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli kuwa ujenzi huo ukamilike ndani ya miezi miwili kuanzia Machi mwaka huu.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Sanare, kwa viongozi alipofanya ziara wilayani humo ya ufuatiliaji wa maagizo ya Rais aliyoyatoa Machi 16 , mwaka huu alipotembelea ujenzi wa Daraja la Kiegeya.

Aliwaagiza viongozi hao akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Kilosa pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kukamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji la kituo hicho ambalo lipo kwenye hatua ya upauaji.

"Hatukumaliza ndani ya miezi miwili, lakini mpo katika hatua nzuri...sasa tukamilishe kwa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha na kukamilisha haraka iwezekanavyo kwa jengo hili, " aliagiza Sanare.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Asajile Mwambambale, alisema maandalizi ya ukamilishaji yameshafanyika na yasipojitokeza mabadiliko ujenzi wa jengo hilo utakamilika mwishoni mwa Mei mwaka huu.

Hivi karibuni Mwambambale alisema halmashauri hiyo ilitarajia kutumia takribani Sh. milioni 100 kujenga jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Magubike, kitakachowezesha kuhudumia wananchi wa kata hiyo na nyingine saba zilizo jirani.

Mwambambale alisema kiasi hicho kilitarajiwa kupatikana kutokana na kubana matumizi katika vifungu mbalimbali kwani hazikuwapo kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 na tayari Sh. milioni 40 zilitengwa kwa ajili ya kazi hiyo na zilihamishiwa katika akaunti ya Serikali ya Kijiji cha Magubike.

Wakati huo huo, mkuu wa mkoa alifanya ukaguzi wa ukarabati wa daraja la Mto Berega na kuwapongeza wahandisi waliokuwa wamekarabati daraja hilo ndani ya siku saba baada ya kubomoka na maji ya mvua.

Mkuu wa mkoa, alisema hatua hiyo imewaondolea wananchi changamoto ya muda mrefu walipokuwa wakiipata ya kushindwa kuvuka kutoka upande mmoja kwenda mwingine ikiwamo na eneo la Hospitali ya Berega.

Hivi karibuni Katibu Tawala wa mkoa huo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, alipofanya ziara eneo la ujenzi wa daraja hilo na kusema kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA ) unahitaji zaidi ya Sh. bilioni saba ili kuwezesha kujengwa daraja kubwa jipya hapo baadaye mara fedha hizo zitakapopatikana.

Daraja hilo limeimarishwa ili kupitisha magari yenye uwezo wa tani tatu hadi 3.5 kwa lengo la kuwawezesha wakazi wa vijiji vya Kata ya Barega na vingine wawe na mawasiliano ya barabara kutoka upande mmoja kwenda mwingine kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii.

Daraja la Barega lilipojengwa mwaka 2013 lilikuwa ni la muda baada ya lililokuwapo awali kusombwa na maji na Julai 2017 baada ya Tarura kuanzishwa, ulifanyika uamuzi wa kuwa na daraja la kudumu.

Kwa mujibu wa wahandisi wa Tarura, daraja hilo lina historia ya maji ya mafuriko kusomba magogo, na kwamba daraja litajengwa kwa nguzo nne na litanyanyuliwa juu zaidi ili kupitisha magogo na kuepusha kuziba wakati wa mvua.

NIPASHE JUMATATU MEI 11, 2020
Nipashe
Spotika



MABEKI WA KATI 10 BORA DUNIANI UK. 12&13



IBRAHIMOVIC

# WANASOKA WA5 BORA WA ZAIDI YA MIAKA 35

## ISIKUPITE

TANGU kuanza kwa zama za Premier League, Wayne Rooney ndiye mwenye pasi nyingi za mwisho 'assists' (103) katika ligi hiyo, akifuatiwa na Dennis Bergkamp (94) na Teddy Sheringham (76).



**LONDON,** England

WACHEZAJI wengi wa soka kiwango chao huwa kinaanza kushuka wanapofikia umri wa miaka 30. Na wengi huamua kustaafu soka katikati ya miaka 30.

Hata hivyo, kuna wanasoka ambao wanakuwa na uwezo wa kucheza hata zaidi ya miaka 35 na kiwango chao kikaonekana kuwa fiti tu.

Makala haya yanawachambua wanasoka ambao wana miaka 35 na zaidi ambao bado wapo fiti dimbani, twende sasa...

**#5. JOAQUIN**

Katika umri wake wa miaka 38, Joaquin ni mchezaji mkongwe zaidi kwenye orodha hii. Ukiacha misimu miwili aliyocheza nchini Italia, raia huyu wa Hispania amecheza kwa misimu 17 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na anashika nafasi ya tatu kama mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi za La Liga.

Nahodha huyu wa Real Betis, msimu huu amefunga mabao 10 katika mechi 28 alizocheza. Msimu huu pia Joaquin amekuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye LaLiga.

**#4. THIAGO SILVA**

Thiago Silva amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora wa kati duniani tangu alipohamia AC Milan mwaka 2009. Raia huyu wa Brazil kwa sasa anacheza pale Paris Saint-Germain, lakini umri wake wa miaka 35, haujamzuia yeye kuwa bora.

**#3. FRANCK RIBERY**

Wakati wake, Franck Ribery alikuwa mmoja wa mawinga hatari zaidi duniani na upatina wake na Arjen Robben pale Bayern Munich ulikuwa na mafanikio makubwa zaidi.

Baada ya misimu 12 ya mafanikio kwa miamba wa Bavaria, Ribery aliamua kwenda Fiorentina kipindi cha majira ya joto mwaka jana.

Katika umri wake wa miaka 37, raia huyu wa Ufaransa bado anaonyesha kuwa na kasi ile ile na fiti katika kukimbia na mpira na kufunga mabao.

**#2. ZLATAN IBRAHIMOVIC**

Unaweza kusema nini kuhusu Zlatan Ibrahimovic? Mchezaji huyu bora zaidi nchini Sweden kwa miaka yote anaonekana kuwa kwenye kiwango kilekile.

Ibrahimovic ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi katika kizazi chake. Amekuwa na wakati mzuri katika timu za Ajax, Juventus, Inter Milan, AC Milan, Barcelona, PSG na Manchester United. Na kwa sasa anacheza kwa kipindi cha pili pale Milan baada ya kujiunga akitokea LA Galaxy ya Marekani wakati wa dirisha la Januari.

Katika umri wake wa miaka 38, ameonyesha kwamba bado ana nguvu kwani pale kwenye dimba la San Siro amefunga mabao manne msimu huu.

**#1. CRISTIANO RONALDO**

Cristiano Ronaldo anaendelea kuwa bora na bora zaidi. Alitimiza umri wa miaka 35, Februari mwaka huu na bado anaonekana kama vile ana umri wa miaka 20.

Mshambuliaji huyu wa Juventus amefunga mabao 25 msimu huu, huku akitikisa nyavu mara 21 katika mechi 22 za Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Amevunja rekodi nyingi msimu huu, ikiwamo ya kufunga mabao katika mechi 11 mfululizo za Serie A. Ronaldo amefuata nyayo za Alexis Sanchez kuwa mchezaji wa pili kufunga hat-trick kwenye Ligi Kuu ya England, La Liga na Serie A.

Ukiangalia kiwango chake na nguvu aliyonayo, Ronaldo haonyeshi kama ataachana na soka hivi karibuni.

Jambo moja la uhakika ni kwamba, Ronaldo hana mpango wa kustaafu soka leo au kesho.

## Extra Time

# MABEKI WA KATI 10 BORA DUNIANI



**LONDON,** England

NI ukweli kwamba, wengi wetu mabao ndio kitu kinachovutia zaidi kwenye mchezo wa soka. Nani asiyependa kuona nyavu zikitikiswa kwa shuti la umbali wa yadi 30? Lakini kushinda mechi mambo mengi yanahitajika kuliko mabao.

**Walinzi wana mchango mkubwa zaidi kwenye mchezo wa soka kwa kuhakikisha washambuliaji hawapiti kirahisi na kufunga mabao.**

Makala haya yanakuchambulia walinzi wa kati 10 bora duniani kwa sasa. Lakini kuna wengine ambao ni heshima kuwataja ambao hawapo kwenye orodha hii akiwamo, Gerard Pique, Thiago Silva, Jerome Boateng na Toby Alderweireld...

### #10. MATS HUMMELS

Staili ya ukabaji ya Mats Hummels ni ya aina yake. Anachukuliwa kama mmoja wa walinzi bora zaidi duniani, kutokana na uwezo wake, kiwango chake kisichoshuka na nguvu aliyonayo.

Uwezo wake wa kutibua mashambulizi ya timu pinzani, na kipaji alichojaliwa ndio kinamfanya kuwa mmoja wa mabeki bora kabisa kwa sasa.

Raia huyu wa Ujerumani amekuwa akifananishwa na gwiji wa soka wa nchi hiyo, Franz Beckenbauer.

### #9. MILAN SKRINIAR

Ilikuwa ni mwaka 2017 ambapo Milan Skriniar alijiunga na Inter Milan kutoka Sampdoria. Raia huyu wa Slovakia amejiimarisha yeye mwenyewe na kuwa mmoja wa walinzi bora zaidi Ulaya pale Nerazzurri.

Ni mchezaji aliyekamilika. Ubora wa Skriniar unajieleza wenyewe wakati akiwa dimbani.

Kama atabakia Inter, Skriniar atakuwa bora na bora zaidi chini ya kocha, Antonio Conte kwa sababu bado ni kijana na ana muda wa kutosha wa kuendelea kuwa fiti.

### #8. LEONARDO BONUCCI

Ukiondoa msimu mmoja usio na mafanikio pale AC Milan, Leonardo Bonucci amekuwa na kiwango kisichoshuka.

Ni mlinzi mwenye nguvu, hodari na raia huyu wa Italia amejitengenezea jina yeye mwenyewe kama beki bora zaidi kwa sasa duniani.

Bonucci si tu kwamba ana uwezo mkubwa wa kukaba, bali pia huwa anapanda na kushuka kwa ajili ya kusaidia mashambulizi mbele ya lango la wapinzani.

### #7. RAPHAEL VARANE

Huyu ni mlinzi aliyeshinda kila kitu kwenye soka. Katika umri wake wa miaka 27, Raphael Varane tayari ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Dunia. Kiujumla raia huyu wa Ufaransa ameshinda mataji 16 makubwa pale Real Madrid tangu alipotua kwenye dimba la Bernabeu kipindi cha majira ya joto mwaka 2011.

### #6. GIORGIO CHIELLINI

Ni mlinzi mwenye akili zaidi dimbani. Licha ya kwamba anatajwa kuwa anacheza kwa staili ya kizamani, lakini ni ngumu mno kumpita anapobaki yeye na mshambuliaji.

Ana nguvu, kasi na uwezo mkubwa wa kuokoa hatari nyingi langoni mwake na uzuri ni kwamba, Giorgio Chiellini ana bahati ya kucheza na walinzi wengi wazoefu na bora barani Ulaya.

Uwezo wake na kasi yake zimekuwa na mchango mkubwa zaidi kwa timu yake na hivyo kujikuta kuwa mmoja wa wachezaji ambaye anacheza mechi nyingi zaidi kwa timu.

### #5. AYMERIC LAPORTE

Aymeric Laporte ni mchezaji tofauti kabisa katika walinzi wa kati wanaocheza kwenye Ligi Kuu ya England. Laporte anasema anamshukuru Pep Guardiola, kwani ilikuwa rahisi kwake kuzoea haraka kucheza kwenye Ligi Kuu ya England.

Kiukweli, Laporte ambaye ni raia wa Ufaransa ni mmoja wa walinzi wazuri zaidi kama Van Dijk linapokuja suala la kukaba.

Laporte ana kasi, nguvu na hodari sana wa kuzuia hatari zote zinazoelekea langoni mwake. Kwa mujibu wa Guardiola, ni mlinzi bora zaidi wa kati duniani anayetumia mguu wa kushoto.

### #4. SERGIO RAMOS

Mchezaji wa mechi kubwa mwenye uwezo mkubwa wa kufunga, ndio kitu ambacho kinamtambulisha Sergio Ramos.

Ramos amebarikiwa kuwa na kasi, nguvu na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira bila kuwa na woga kwa washambuliaji.

Pia ana uwezo mkubwa wa uongozi anapokuwa dimbani na hilo limemfanya kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi kuwahi kutokea katika soka la Hispania.

Ramos amekuwa akicheza katika daraja la juu kwa miaka mingi na kiwango chake kimekuwa katika ubora ule ule.

### #3. DIEGO GODIN

Staili ya uchezaji ya Diego Godin ni ya kuvutia sana. Alikuwa na wakati mzuri sana wakati wa kipindi chake cha uchezaji pale Atletico Madrid akiwa chini ya kocha, Diego Simeone.

Kwa sasa akiwa pale Inter Milan, Godin huwa haoni shida kuulaza mwili wake wakati akiokoa hatari yoyote langoni mwake. Uwezo wake na kazi zimemfanya kuwa mmoja wa walinzi bora zaidi duniani kwa sasa. Ana nguvu na uwezo mkubwa wa kucheza mipira ya kichwa langoni mwake na huwa anapanda kusaidia mashambulizi kwa timu yake.

### #2. KALIDOU KOULIBALY

Mwili wake unajielezea mambo mengi. Ni imara, ana nguvu na kasi kubwa anapokuwa dimbani. Licha ya kuwa mmoja wa walinzi wenye mwili mkubwa, Koulibaly amejiimarisha yeye mwenyewe kuwa beki bora kabisa katika soka la kisasa.

Raia huyu wa Senegal urefu wake umekuwa nguzo kubwa ya kucheza mipira ya kichwa na pia kuzuia mashambulizi langoni mwake.

Kwa sasa ameweka historia ya kuwa mlinzi bora zaidi katika Ligi Kuu ya nchini Italia akiwa anakipiga pale Napoli.

### #1. VIRGIL VAN DIJK

Wakati Liverpool wakimsajili mlinzi huyu hakuna aliyewahi kufikiria kwamba atakuja kufanya makubwa ndani ya klabu hiyo. Virgil Van Dijk raia wa Uholanzi amekuwa na muda wa kuvutia zaidi tangu atua pale kwenye dimba la Anfiled.

Ni mlinzi ambaye anajua kumpigia hesabu mpinzani wake na uzuri ni kwamba hata kwenye pasi yuko vizuri. Amecheza kwa mafanikio makubwa zaidi Liverpool licha ya kukaa hapo kwa muda mfupi. Kwa sasa anatajwa kama mmoja wa walinzi bora zaidi kuwahi kucheza kwenye Ligi Kuu ya England.

Urefu wake, nguvu na kasi zimekuwa na mchango mkubwa zaidi kwa timu yake na huwa haishangazi kuona kwamba washambuliaji wengi bora barani Ulaya wamekuwa wakimgwaya na kumwelezea kama ni beki mgumu mno kumpita na mpira.


Van Dijk pia ana kila kitu ambacho mlinzi anatakiwa kuwa nacho hasa linapokuja suala la ubunifu na uwezo binafsi dimbani.

Van Dijk ana kila kitu kwa walinzi wa soka la kisasa, kasi nguvu na uwezo wa kumzuia mshambuliaji yeyote anapoingia kwenye himaya yake.

KOULIBALY

## Nukuu

"Bado ana miaka mizuri mitano au saba ya kuendelea kucheza, anajitunza sana na anaweza kuendelea kucheza hadi akiwa na umri wa miaka 37, 38 au 39. Atacheza michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar, nina uhakika," **Xavi akimzungumzia Lionel Messi wakati wa mahojiano mubashara kupitia Instagram na mshambuliaji wa zamani wa Barca, Samuel Eto'o**



"Kama wana nguvu ya kiuchumi wanaweza kumpata, wanatakiwa kufanya haraka, ni kweli hajawa kwenye ubora wake kwa misimu ya hivi karibuni, lakini atarudi kwa nguvu kwa sababu anajua soka vizuri na hatahitaji kuanza kuzoea mazingira. Kutokana na uwezo wake na kipaji alichonacho atazoea haraka sana kwenye Serie A," **gwiji wa Inter Milan, Giuseppe Bergomi akiliambia gazeti La Gazzetta dello Sport kuhusu klabu hiyo kumsajili Paul Pogba.**



"Kama ningekuwa mimi ningebakia Inter, pale Barcelona atasugua benchi," **Kocha wa zamani wa Real Madrid, Fabio Capello akitoa ushauri kwa nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez kutojiunga na Barca.**



# LIGI KUU IKIREJEA TUTARAJIE HAYA 7



Beki wa kushoto wa Simba, Gadiel Michael ambaye yupo kwenye ushindani mkubwa wa namba dhidi ya mchezaji mwenzake, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr'. **PICHA: MAK-**

**Na Adam Fungamwango**

TAYARI Bodi ya Ligi imetangaza kuwa kama mambo yakienda kama yalivyopangwa kwa kupata baraka za kurejea kwa ligi nchini kutoka serikalini, huenda Ligi Kuu Tanzania Bara ikaendelea tena kutimua vumbi Juni mwaka huu.

**Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na michezo yote kwa ujumla ilisimamishwa rasmi na serikali Machi 17, mwaka huu, baada ya dunia kukumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.**

Lakini matarajio ya kurejea kwa ligi hii sasa yanakuja baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kusema kuwa anafikiria kuruhusu mechi za ligi kuendelea.

Baada ya tamko hilo, Bodi ya Ligi ikaja na kauli kuwa wanasubiri kwa hamu, rais ashauriane na wataalamu wake ili ligi irejee na huenda ikawa Juni kama mambo yataenda kama yalivyopangwa.

Kwa sababu imesimama kwa muda sasa kutokana na ugonjwa wa COVID-19, ikirejea kuna baadhi ya mambo ambayo huenda yakajitokeza kwa muda mfupi au yakawa endelevu, haya hapa...

**1. WACHEZAJI KUTOKUWA KWENYE KIWANGO**

Ligi Kuu Tanzania Bara itakaporejea tena, tunaweza kushuhudia baadhi ya wachezaji wasiwe kwenye viwango vya kawaida, vilivyozoeleka.

Hii ni kwa sababu ya mazoea ya wachezaji wengi wa Kibongo kufanya mazoezi pale wanaposimamiwa tu, lakini wanapokuwa peke yao, ama hawafanyi kabisa, au wanafanya kwa kuzuga tu.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wachezaji watarejea wakiwa wamezidi uzito kutokana na uduni wa mazoezi, lakini na vyakula, hivyo wanaweza kuwa wazito na kuchoka haraka wanapokuwa uwanjani.

Hivyo, mashabiki watarajie kunaweza kuwa na mabadiliko ya wachezaji waliowazoea kuwa mastaa, wasiwe kama walivyowazoea. Labda baada ya muda fulani wanaweza kurejea tena.

**2. WACHEZAJI WALIOFANYA MAZOEZI WATAKIMBIZA**

Itakuwa ni 'hatari na nusu' kwa wachezaji ambao ni kweli muda wote walikuwa majumbani wakipambana ili kujiweka fiti. Ligi Kuu itakaporejea tunaweza kushuhudia baadhi ya wachezaji ambao hatukuwadhania, wakiibuka na kusumbua. Si kwa sababu wana uwezo mkubwa na vipaji sana, la hasha. Ila ni kwa sababu watakuwa wako fiti kimwili, wakipambana na wachezaji goigoi ambao hawakuwa wanafanya mazoezi ya kujiweka vizuri.

Wachezaji wa aina hii watasumbua sana kwenye kipindi hiki cha kumalizia ligi.

**3.WACHEZAJI KUACHWA AU KUSAJILIWA**

Ni kipindi ambacho baadhi ya wachezaji waliokuwa fiti na kufanya vizuri watakuwa wamejiwekea mazingira mazuri ya kupata tena mikataba kwenye klabu zao au kuchukuliwa na klabu zingine kutokana na uwezo watakaouonyesha.

Hali itakuwa tofauti kwa wachezaji ambao walikuwa wamejibwetesha, kwani kama hawatofanya vema, watakuwa wamejiweka kwenye mazingira magumu, si kupata tena mikataba kwenye klabu zingine baada ya ligi kwisha, bali hata zile wanazozichezea kwa sasa. Ni kwa sababu klabu zetu zinaeleweka kwa kupenda zaidi wachezaji ambao wako kwenye viwango vya juu kwa wakati huo.

**4. BAADHI YA WACHEZAJI, MAKOCHA KUTOREJEA**

Imeelezwa kuwa baadhi ya makocha na wachezaji bado wako kwenye nchi zao wakiwa majumbani. Kila nchi ina utaratibu wake. Kuna nchi bado wananchi wao wamezuiliwa kutoka majumbani. Hivyo, hali kama hiyo ikiendelea inawezekana kabisa baadhi yao wasirejee katika klabu zao kwa kipindi hiki.

**5. MATOKEO YASIYOTARAJIWA**

Kingine tunachoweza kushuhudia kwenye ligi hiyo ni matokeo yasiyotarajiwa. Ni kwamba kuna baadhi ya timu zinaweza kupata matokeo wasiyoyatarajia kutokana na wachezaji wao kukaa muda mrefu bila kucheza soka.

Zile timu zilizozoea kushinda zinaweza kupata tabu kupata ushindi na zile zilizoonekana kuwa ni dhaifu zikawa zinapata ushindi. Tunaweza kushuhudia timu zinazoshuka daraja zikawa siyo zile ambazo wengi walizipa nafasi hiyo.

**6. WACHEZAJI WA MAJUKWAA ITAKULA KWAO**

Kwa asilimia zote, inaonyesha kuwa mechi za kumalizia zitachezwa bila mashabiki. Ingawa ni kweli kucheza bila mashabiki kunapunguza ladha, lakini kuna baadhi ya wachezaji wanaweza kuathirika zaidi na hilo. Ni wale wenye kupenda kupaka rangi mpira ili washangiliwe.

**7. MASHABIKI KUJAZANA VIBANDA UMIZA**

Licha ya serikali kupiga marufuku mikusanyiko ili kuepuka kasi ya maambukizo ya virusi vya corona, kutokana na kutoona soka kwa muda mrefu na hamu ya kushuhudia timu zao, wengi watakuwa wanajazana kwenye vibanda umiza, baa na hotelini kwa ajili ya kuangalia mechi za ligi, hali ambayo kila mtu anapaswa kuchukua tahadhari binafsi.

**JE, WAJUA?**



NAHODHA wa Real Betis ya Hispania, Joaquin (38), msimu huu ameshafunga mabao 10 katika mechi 28 alizocheza, pia amekuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye LaLiga.



## HABARI DODOMA

# Yatima wahifadhiwa kanisani kisa mafuriko kubomoa nyumba yao

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MCHUNGAJI wa Kanisa la United Methodist Mbabala 'B', Jiji la Dodoma, Yoram Isihaka, ameamua kuwalea na kuwahifadhi watoto yatima 135 ndani ya kanisa hilo kutokana na nyumba waliyokuwa wakiishi kubomolewa na mafuriko.

Kutokana na hali hiyo, shughuli za ibada za kanisa hilo kwa sasa zinafanyika chini ya mti hadi hali itakapotengemaa.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ametoa msaada wa vyakula, malazi na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa bweni la watoto hao.

Akizungumza alipokuwa akipokea msaada huo, mchungaji huyo alisema mwaka 2001 alianzisha kituo cha kuwalea watoto hao, ambapo kilianza na watoto saba, lakini kwa sasa wapo 135 na walikuwa wakiishi kwenye nyumba iliyojengwa kwa udongo.

"Nina nia ya kuwasaidia watoto kuna wengine wamefanikiwa, nahudumia watoto wote bila kujali dhehebu la mtu, tunalenga kusaidia watoto wasome, hili ni kanisa kwa sasa wanatumia kwa muda kutokana na nyumba ambayo tulijenga kwa ajili ya kuishi kubomoka kwa mvua," alisema.

Alibainisha kuwa amekuwa akiwatunza watoto hao kwenye nyumba iliyokuwa imejengwa kwa udongo, baada ya mvua kubwa za mwaka huu ilibomoka na hivyo watoto hao pamoja na yeye kukosa malazi.

"Hatua hii ilinilazimu kuwaomba waumini kuligeuza kanisa kama nyumba ya kuwahifadhi watoto hawa yatima na wao kusali chini ya mti mpaka hali itakapotengemaa," alifafanua.

Akitoa msaada huo, Mavunde alisema alifikishiwa habari za maisha ya mchungaji huyo na vijana wa Kata ya Kilimani na kuomba kuwaunga mkono kumsaidia.

"Kwa neema ya Mungu leo nimekabidhi magodoro 20, sukari kilo 40, sabuni boksi 10, unga wa ugali kilo 100, sabuni za maji lita 40, ndoo za kunawia mikono, tofali 2,000, saruji mifuko 20 kwa ajili ya kujenga bweni jipya la watoto, na tutamlipa fundi ili watoto wakae kwa nafasi na kutenganishwa wa kiume na wa kike," alisema.

Alisema anachokifanya mchungaji huyo ni zaidi ya ibada ya kawaida, na kwamba wapo watu wenye uwezo mkubwa sana, lakini hawajawahi kufikiri kusaidia watu wenye mahitaji.

"Umeamua kupoteza rasilimali zako kwa ajili ya hawa watoto na hili la kubadilisha nyumba ya ibada ni jambo kubwa la kimungu, watu wanasali nje wanasali kwa imani kwa kuwa unafanya jambo la kimungu," alisema.

Aliahidi kuendelea kumsaidia na kutafuta wadau wengine ili kusaidia watoto hao hasa wanaosoma wapate vifaa vya shule.

# Wanawake Kiislamu wafundwa uvaaji mavazi Mwezi Mtukufu

**Na Peter Mkwavila, KONDOA**

WANAWAKE wa dini ya Kiislamu wa wilaya za Kondoa na Chemba mkoani Dodoma, wameshauriwa kuendelea kuvaa mavazi ya stara kwa kipindi chote, badala ya kuvaa kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani peke yake.

Ushauri huo ulitolewa jana na kiongozi wa dhehebu la Shia Ithnna - Shari Shekhe Abdullatwifu Swalehe, wa msikiti wa wilaya za Kondoa na Chemba, alipokuwa akitoe elimu ya dini ya kiislamu kwa waumini wa Shia.

Alisema mavazi hayo ya stara yanatakiwa kuvaliwa na wanawake kwa kipindi chote na siyo kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu peke yake.

Shekhe huyo alisema wanawake kwa muda wote wawe kwenye mazingira ya nje au nyumbani lazima kuvaa mavazi yenye stara ikiwa ni misingi mizuri ya dini hiyo.

Aidha, kiongozi huyo aliwataka vijana wa dhehebu hilo kutumia mwezi huo kusoma na kuhifadhi Quran Tukufu badala ya kukaa vijiweni na kucheza kamari na kuimba nyimbo za kidunia.

"Tumieni muda wenu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, kusoma na kuhifadhi Quran, badala ya kukaa huko vijiweni ambako kumekuwa ni sehemu ya vitendo viovu kwa vijana walio wengi," alisema.

Kadhalika, aliwataka waumini hao kuunga juhudi za Rais John Magufuli katika kuwaelimisha na namna ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Aidha, aliwataka kuchukua hatua za kujilinda na ugonjwa huo na kutoa elimu kwa wengine bila kujali itikadi ya mtu yoyote kwa kuwa ugonjwa hauchagui dini wala kabila.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde (aliyevaa kofia), akimkabidhi Mchungaji wa Kanisa la United Methodist la Mbabala B jijini Dodoma, Yoram Isihaka, msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya watoto yatima anaowalea.

# Wizara yatakiwa kuongeza kasi ya usambazaji gesi majumbani

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Nishati imetakiwa kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi majumbani ili kuwanufaisha wananchi na kuwapunguzia gharama za maisha.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki bungeni na Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alipokuwa akichangia bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2020/21.

Chikota alisema miradi mingine ya umeme imesimamiwa kikamilifu, lakini usambazaji gesi majumbani bado kasi yake hairidhishi.

"Hadi sasa gesi imefika kwa vijiji 425, lakini kuna mitaa mingine ya Mangowela ambayo yapo maeneo yaliyotakiwa kufikiwa, lakini nashangaa mitaa hii kutofikiwa," alisema.

Alisisitiza gesi majumbani mchakato wake bado haukidhi mahitaji hivyo kasi iongezwe.

Awali, akiwasilisha bajeti, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema Sh. bilioni 10.1 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya usambazaji wa gesi kwenye Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Dk. Kalemani alisema serikali inaendelea na kazi za kusambaza gesi asilia kwa wateja wote walio karibu na miundombinu ya usambazaji katika mikoa hiyo.

Alisema kazi zilizotekelezwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia yenye urefu wa kilomita 17 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 3,000 kwa Mkoa wa Mtwara.

"Wateja hao ni katika maeneo ya Chuo cha Ufundi, Chuo cha Ualimu Mtwara, Sekondari ya Ufundi na Gereza la Lilungu na Mitaa ya Magomeni, Shangani, Reli, Chikongola na Tandika, hadi sasa, nyumba 425 zimefikiwa na miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia na uunganishaji unaendelea," alisema.

Aidha, alisema katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira katika mikoa hiyo, kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita 7.8 kutoka kwenye bomba la usafirishaji gesi asilia hadi Mnazi Mmoja – Lindi.

"Pia ununuzi wa mtambo wa kupima kiwango cha gesi, kupunguza msukumo na kuweka harufu kwa ajili ya usalama, mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Manispaa ya Lindi kupitia Mnazi Mmoja ambapo takriban wateja wa awali zaidi ya 1,000 watakaounganishwa na Sh. bilioni 10.1 zimetengwa," alisema.





# Chawata yaahidi kuenzi mchango wa Dk. Mengi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

CHAMA cha Watu wenye Ulemavu (Chawata), Mkoa wa Mbeya, kimesema kuwa daima kitaendelea kuenzi na kukumbuka mchango wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, marehemu Dk. Reginald Mengi, katika kulisaidia kundi hilo kwa maelezo kuwa kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa Covid-19 angewapatia msaada wa vifaa kinga.

Kimesema kwa sasa wanakabiliwa na changamoto ya mahitaji kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya corona, na kwamba hawajapokea msaada wowote kutoka kwa wadau, hivyo kumkumbuka Dk. Mengi.

Hayo yalibainishwa jana na Makamu Mwenyekiti wa Chawata, ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho mkoani Mbeya, Jimmy Ambilikile, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema hadi sasa kundi hilo halijapokea msaada wowote wa vifaa, lakini walipata habari katika maeneo mbalimbali mkoani humo wanapatiwa.

Alisema chama hicho kina uhitaji mkubwa wa vifaa vya kujikinga na corona kutokana na hali walizonazo, ambazo kwa namna moja au nyingine zinasababisha washindwe kumudu gharama za kununua.

"Chawata kinawaomba wadau na serikali kuwasaidia vifaa vya kujikinga na corona... kundi hili liko kwenye hatari ya kupata ugonjwa huo, kutokana na hali tulizonazo, wakati huu ni mgumu kwetu unasababisha kumkumbuka rafiki na ndugu yetu marehemu Dk. Mengi najua angetupatia msaada hakika tutaendelea kumkumbuka daima," alisema Ambilikile.

Aliongeza kuwa kutokana na ugumu wa maisha, ofisi ya chama hicho mkoa, imeshindwa kuwa hata na ndoo ya maji kwa ajili ya kunawa mikono.

Alisema Mkoa wa Mbeya una jumla ya watu wenye ulemavu 900, na kwamba wengi wao wanaishi kwenye mazingira magumu.

Mwenyekiti wa Chama hicho Jiji la Mbeya, Damas Mwambeje, aliomba serikali kuendelea kutoa elimu ya namna ya kujikinga kwa kundi hilo kwa maelezo kuwa wengi bado hawana uelewa wa kutosha.

"Tumekuwa tukipata taarifa kuwa kwa mkuu wa mkoa wadau mbalimbali wanapeleka vifaa vya kujikinga na corona, lakini sisi hatujawahi kuletewa sasa sijui wanampangо gani, maana maeneo mengine tayari wamepatiwa hadi CCM tunaomba na sisi tukumbukwe maana hii vita ni yetu sote," alisema Mwambeje.

Aliongeza kuwa hata vifaa vilivyowekwa kwenye taasisi mbalimbali za umma sio rafiki kwao, hivyo kuwa kwenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa huo.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akipokea msaada wa lita 500 za vitakasa mikono kutoka kwa Meneja wa kiwanda cha TBL Plc mkoani humo, Godwin Fabian (kulia), vilivyotolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa COVID 19, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito waonywa unywaji wa pombe

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, amewaonya wajawazito kuacha matumizi ya pombe ambayo yanatajwa kama aina ya ukatili kwa mtoto aliyeko tumboni.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake ambapo alisema wajawazito wanaokunywa pombe watambue kuwa wanawafanyia ukatili watoto walioko tumboni ambao kimsingi hawana hatia.

Kisemba, alisema aina hiyo ya ukatili kwa mtoto aliyeko tumboni huchangiwa na mambo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa elimu juu ya athari za unywaji pombe, wajawazito kuamini unywaji wa pombe uimarisha afya ya mtoto tumboni, lakini wengine ni walevi hivyo hushindwa kuacha wakishika mimba.

"Unywaji wa pombe kwa mama mjamzito ni kosa na miongoni mwa aina za ukatili, dhidi ya mtoto aliyeko tumboni ambaye kupitia pombe hizo anaweza kupata udumavu ambao utamsababishia madhara ya kimwili na kifikra," alisema Kisemba.

Alisema mtoto atakapozaliwa anaweza kukosa uwezo wa kufikiri vizuri na kumpelekea kuwa zezeta kutokuwa mchangamfu, lakini pia hatua zake za ukuaji zitakuwa za kusuasua.

Aliwaomba kuacha matumizi ya pombe, lakini pia wadau vikiwamo vituo vya taarifa na maarifa kuendelea kutoa elimu juu ya athari hizo na kufuata ushauri wa kitaalamu.

Alisema vituo vya taarifa na maarifa kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwamo TGNP- Mtandao kuelimisha jamii aina za ukatili wa kijinsia, malezi na makuzi kwa mtoto.

Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi alisema wajawazito wengi wanaokunywa pombe ni mabinti ambao kimsingi hawana elimu ya kutosha kuhusiana na afya ya uzazi.

# Rungwe wajivunia kunufaishwa na kiwanda cha maji

**Na Grace Mwakalinga, RUNGWE**

WANANCHI wa Kijiji cha Kibisi, Kata ya Kimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wamesema wamenufaika na uwapo wa kiwanda kipya cha maji.

Wamesema mbali na kuwa na uhakika wa huduma ya maji, lakini wameboreshewa barabara na kupata ajira.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa wananchi hao, Tusekile Mwakanosya, alisema mmiliki wa kiwanda hicho amewasaidia kuwatengenezea barabara kuzunguka kijiji hicho.

Alisema awali barabara hiyo ilikuwa ni tatizo kwao hasa msimu wa mvua kutopitika kwa urahisi ukilinganisha na sasa ambapo hadi magari yanapita kwa urahisi.

"Kibisi ya miaka ya nyuma sio ya sasa maana tunashuhudia maendeleo kila uchao, tunamshukuru mmiliki wa kiwanda cha maji kuja kuwekeza kijijini kwetu... hakika kafungua fursa mbalimbali hasa kwetu kinamama tumefungua biashara zetu, lakini tumepata ajira za muda mfupi, tunauwezo wa kijikimu," alisema Mwakanosya.

Kaimu Meneja wa Kiwanda hicho, Gwandumi Mpoma, alisema lengo la kuanzisha kiwanda hicho cha maji kijulikanacho kama Tukuyu Spring ni kufungua fursa za kiuchumi kwa wakazi wote wa Mji wa Tukuyu.


Alisema wanafanya hayo ili kuunga mkono jitihada za serikali za kufikia azma ya viwanda, ambayo itaisaidia serikali kuongeza mapato, lakini kuongeza ajira kwa vijana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Ahobokile Kabungo, alieleza kuwa alimua kufungua kiwanda hicho nyumbani kwao kama sehemu ya kurudisha fadhila.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ezekiel Mwankota, alisema wilaya hiyo ina fursa nyingi za kiuchumi, hivyo anakaribisha wadau wengi kuwekeza.

Alisema Rungwe inatekeleza sera ya serikali kuelekea Tanzania ya viwanda, ambapo baadhi ya viwanda vinafanya kazi vikiwamo viwanda vya kusindika chai.

**"Kibisi ya miaka ya nyuma sio ya sasa maana tunashuhudia maendeleo kila uchao, tunamshukuru mmiliki wa kiwanda cha maji kuja kuwekeza kijijini**



## SMZ: Zanzibar haiwezi kujiunga OIC kwa sasa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama na kujiunga na Jumuiya ya Kimataifa ya Kiislamu (OIC) kwa sababu sifa za kujiunga na taasisi hiyo ni nchi yenye uwakilishi kamili wa Jamhuri.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi, wakati akijibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Ussi alisema Zanzibar ilifanya jaribio la kujiunga na OIC mwaka 1992, lakini alilazimika kujiondoa kwa sababu Zanzibar haina uwakilishi wa Jamhuri kwa maana ya dola kamili inayojitegemea.

"Kitendo cha Zanzibar kujiunga na OIC kilionekana wazi wazi kwamba ni ukiukwaji wa katiba kwa sababu mambo ya ushiriki wa Jumuiya za Kimataifa upo chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alifafanua.

Ussi alikuwa akijibu hoja za Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Mohamed Raza, aliyetaka kujua kwa nini Zanzibar haijiungi na OIC kama ilivyofanya mwaka 1992 ili kufaidika na misaada na huduma mbalimbali zinazotolewa na jumuiya hiyo.

Alisema suala hilo limejadiliwa na kuonekana kwamba muda mwafaka ukifika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itajiunga na jumuiya hiyo.

Zanzibar ilijaribu kujiunga na OIC wakati katika uongozi wa Rais Dk. Salmin Amour Juma, lakini ililazimika kujiondoa baada ya kufanya hivyo bila baraka za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo kukiuka katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Uamuzi huo ulisababisha baadhi ya viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuondolewa katika nafasi zao kutokana na kutowajibika.

OIC ilianzishwa mwaka 1969, huku ikiwa na wanachama 57, ambapo wanachama 53 ni nchi zenye idadi kubwa ya wafuasi waumini wa dini ya Kiislamu.

**"Kitendo cha Zanzibar kujiunga na OIC kilionekana wazi wazi kwamba ni ukiukwaji wa katiba kwa sababu mambo ya ushiriki wa Jumuiya za Kimataifa upo chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alifafanua.**

# Corona yawa fursa kwa wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman**

LICHA ya ugonjwa wa corona kusababisha kushuka kwa uchumi, lakini wajasiriamali wanaotengeneza sabuni za maji imekua ni fursa kwao katika kuongeza kipato.

Wakizungumza na Nipashe, walisema wanapokea tenda kutoka kwa watu mbalimbali wanaohitaji bidhaa hiyo ambayo ni moja wapo inayotumika katika kujikinga na corona kwa kuosha mikono kwa kutumia sabuni na maji.

Zeyana Seif Salum kutoka kikundi cha wajasiriamali cha Msawika kilichopo Bambi Wilaya ya Kati Unguja, alisema licha ya kuwa ugonjwa wa corona ni janga la dunia, lakini kwa upande wao ni fursa ambayo imesaidia kuuza bidhaa zao kwa wingi kipindi hiki.

"Corona kwetu imekuwa ni fursa kubwa maana kabla hatukuwa na soko la sabuni, lakini sasa soko ni zuri sabuni za maji zinahitajika kwa wingi," alisema.

Alieleza kuwa sabuni wanazotengeneza zina ubora na wanafuata maelezo kutoka kwa taasisi za viwango na bidhaa zao zimekuwa zikikubalika.

Naye Sada Muhamed kutoka Kijiji cha Mtende Mkoa wa Kusini Unguja, alieleza kuwa kabla ya corona kipato walichokuwa wakipata kilikua kidogo kwa sababu wananchi walikuwa hawajahamasika kununua sabuni hizo badala yake baadhi ya ofisi ndio zilizokuwa zikitumia na wengine walikuwa wakiagiza kutoka nje ya nchi.

Alisema hivi sasa katika janga la corona jamii imehamasisha kutumia sabuni na wanapokea oda nyingi kutoka kwa taasisi mbalimbali.

Aliwataka wajasiriamali wenzake kuitumia fursa hiyo na kutengeneza sabuni zenye ubora na pia kutopandisha bei kuwakomoa wananchi kwa lengo la kutaka kupata faida kubwa.

Alieleza kuwa elimu ya utengenezaji sababu wameipata kwa wasimamizi wa mradi unaondeshwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania Tamwa Ofisi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Taasisi ya Milele Foundation ambao waliwatafutia wataalamu kuwapatia elimu na vifaa vya utengenezaji sabuni.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Zanzibar (SMIDA), Shadida Ali Salum, alisema baada ya kuzuka kwa corona, waliwakusanya wajasiriamali kuwapatia mafunzo ya utengenzaji wa sabuni na vitakasa mikono, ili kuweza kutengeneza kwa wingi ambapo hivi sasa vimekuwa na mahitaji makubwa.

Aliwataka wajasiriamali kufika SMIDA kwa ajili ya kupata mkopo wa fedha ili kuweza kuagiza vifungashio ambavyo vimekua na changamoto katika upatikanaji wake.

Alieleza kuwa wapo wajasiriamali wanaotengeneza sabuni za maji ambazo ni nzuri na zimekuwa na viwango vinavyokubalika.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, aliwataka wajasiriamali hasa wanawake kuongeza nguvu ya uzalishaji wa bidhaa wanazotengeneza ikiwamo sabuni ya maji, vitakasa mikono na barakoa ambavyo vimekua na soko kubwa katika kipindi hiki cha corona.

Akizungumzia kuhusu changamoto ya vifungashio alisema upo uhaba wa vifungashio hasa chupa za kuwekea sabuni za maji hivyo serikali itahakikisha inalifanyia kazi ili kuweza kupatikana kwa wingi.



Katibu Mwenezi wa CCM tawi la Shangani Zanzibar, Rose Martin Kabemba (kushoto), akizungumza na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Tawi hilo, Kiran Chagan Mawji (hayuko pichani), baada ya ujumbe wa chama wa tawi la hilo kumtembelea ofisini kwake, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mwanafunzi aliyebakwa ajifungua salama

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza aliyebakwa na kupewa ujauzito, amejifungua salama, huku matarajio yake ni kuendelea na masomo baada ya shule kufunguliwa.

Mwanafunzi huyo (jina tunalihifadhi), alibakwa na jirani yake mwenye umri miaka 25 na kumpa ujauzito, ambapo mtuhumiwa aliiomba familia ya mwanafunzi huyo kwa lengo la kutaka kumuoa ili kesi isifike katika vyombo vya sheria.

Mama wa mwanafunzi huyo, alisema kitendo cha kubakwa na kupewa ujauzito mtoto wake ambaue anaumri wa miaka 16 kimemsikitisha sana na hakukubaliana na ombi la mtuhumiwa, hivyo aliamua kesi hiyo kuipeleka katika vyombo vya sheria.

"Nilimgundua mtoto wangu akiwa na mimba miezi mitano na Mei 3 amejifungua mtoto wa kiume... kesi ipo polisi sijui imefikia wapi, maana kila nikienda kituo cha polisi kufuatilia sijaridhika na maelezo ninayopewa," alisema.

Alieleza kuwa baada ya mtoto wake kugundua kufanyiwa kitendo hicho na kumtaja mtuhumiwa, aliripoti kituo cha Polisi Mwera, lakini anashangaa kuona familia ya mtuhumiwa ilimfuata na kutaka kesi hiyo waimalize kienyeji ili mtoto wake aolewe na mtuhumiwa.

Alisema alikataa kwa sababu tayari kesi hiyo ameshaifikisha katika vyombo vya sheria, hivyo ameviomba vyombo hivyo kuhakikisha kesi hiyo inatendewa haki.

"Mtoto wangu bado mdogo sitaki aolewe, nataka aendelee na masomo na kwa kuwa sheria inaruhusu mtoto aliyepata ujauzito kuendelea na masomo, nasubiri shule zifunguliwe ili aendelee na masomo," alisema.

Naye Mkuu wa Dawati la Jinsia Polisi Mwera, Jamali Muhammed, alisema kesi hiyo namba IR 141/2020 inaendelea kufanyiwa upelelezi, na jalada lipo katika ngazi za Polisi mkoa kwa ajili ya hatua zaidi.

Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Kombo Khamis, alisema jalada limeshakamilika upelelezi wake na hivi sasa lipo katika hatua la kulifikisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya hatua zingine.

Akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina, ofisa mmoja katika ofisi ya DPP, alisema ofisi hiyo imesitisha kupokea majalada ya kesi kwa sababu ya ugonjwa wa corona.

Meneja wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa)-Zanzibar, Asha Abdi, alisema hali hiyo itapelekea ucheweleshwaji wa kutoa haki kwa kesi za udhalilishaji, ambazo waathirika wake wanazidi kuathirika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**CHAMPION AUCTION MART P.O.BOX 4080 DAR**

**KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UNITY 3E SOLUTION(T) LIMITED MWANZA, TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA YA MKOPO WA WADAIWA WAO AMBAZO NI NYUMBA, KIWANJA, GARI IWAPO MDAIWA HATALIPA DENI NDANI YA SIKU KUMI NA NNE(14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI**

1] MDAIWA-CHARLES MAKANYAGA,DHAMANA- TOYOTA SURF T.846 BGY, MAHALI-MKOLANAI,TAREHE 13/5/2020 SAA 4 ASUBUHI
2] MDAIWA –LUSSAGA BILIA LUSSAGANA, DHAMANA- TOYOTA LAND CRUISER T.693 BGB, MAHALI-MKOLANAI,TAREHE 13/5/2020 SAA 4 ASUBUHI
3] MDAIWA- BALTAZARY EVERIST KIPEJA, DHAMANA- TOYOTA BREVIS T. 194 DJQ, , MAHALI-MKOLANAI,TAREHE 13/5/2020 SAA 4 ASUBUHI
4] MDAIWA- MARTIN FRANCIS MAKOYE,DHAMANA- TOYOTA (TX PRADO) T.178 BAE, , MAHALI-MKOLANAI,TAREHE 14/5/2020 SAA 4 ASUBUHI
5] MDAIWA- MONICA SIMBO, DHAMANA- NISSAN MURANO T.777 DEF, MAHALI-MKOLANAI,TAREHE 14/5/2020 SAA 4 ASUBUHI
6] MDAIWA- PETER SALVATORY NGUNGA,DHAMANA- TOYOTA KLUGER T.162 DPB, MAHALI-MKOLANAI,TAREHE 14/5/2020 SAA 4 ASUBUHI
7] MDAIWA- CATHERINE ZACKARIA RINGO, DHAMANA- KIWANJA, MAHALI- BUHONGWA(NYAKAGWE), TAREHE 19/05/2020 SAA 5ASUBUHI
8] MDAIWA- ELIZABETH JEMES DHAMANA-KIWANJA, MAHALI-BUHONGWA, TAREHE 19/05/2020 SAA 7MCHANA
9] MDAIWA- DASTAN B KAMUGISHA, DHAMANA- KIWANJA, MAHALI-USAGALA FELA(MISUNGWI), TAREHE 20/05/2020 SAA 4 ASUBUHI
10] MDAIWA- HAMISA, DHAMANA- KIWANJA, MAHALI- LWANHIMA, TAREHE-21/05/2020
11] MDAIWA- STEVEN MABULA,DHAMANA- NYUMBA, MAHALI-BUYOMBE (KISEKE), TAREHE 15/05/2020 SAA 9 MCHANA
12] MDAIWA - MOHAMED ALLY SAID, DHAMANA- NYUMBA NA KIWANJA, MAHALI- LWANHIMA, TAREHE 21/05/2020 SAA 7 MCHANA
13] MDAIWA- NYANGANYI ELIAS FINIAS, DHAMANA- NOAH VOX T.470 DNQ, MAHALI- MKOLANI, TAREHE 14/05/2020 SAA 6 MCHANA

157367

## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)

Katika Mahakama ya Mwanzo **MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa Mirathi **Na. 105/2020**

Ombi la **REHEMA HOSIANA MWAKATUMBUGA** kuteuliwa

Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu
**HOSSIANA CHARLES MWAKATUMBUGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 27/05/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 27/04/2020.

157368

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA MASWA
MAHALI MASWA
MAOMBI NAMBA 25 YA MWAKA 2020
KATI YA

OKEYA MWITA OKEYA…………..MWOMBAJI
DHIDI YA

1. BARAKA FELIX ALPHAYO
2. ROSIER P. NKOBERO …………WAJIBU MAOMBI

**WITO / TAARIFA**

KWA: BARAKA FELIX ALPHAYO NA ROSIER P. NKOBERO POPOTE MLIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yenu katika Baraza hili la wilaya ya Maswa. Maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani. Mnatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wenu wa maandishi (WSD) kabla ya tarehe 02.06.2020.
Pia mnajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 02.06.2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. J.F. Kanyerinyeri, Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya – Maswa.
Pia mnafahamishwa kuwa iwapo mjitahidi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yenu.

157364

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA
Usimamizi wa Mirathi NAMBA 60/2020
Ombi la MWAKAMA OMARI JABIR
kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi marehemu
SALIMU MOHAMEDI MSELEMU

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 27/5/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 05/05/2020

Sahihi ya Hakimu

157369

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Chuo chavumbua mfumo upimaji corona

**NAIROBI,** Kenya

TANGU mlipuko wa virusi vya corona, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanyika ili kuzuwia kusambaa kwa virusi hivyo ambavyo vinaambukizwa kwa kasi duniani na kusababisha vifo.

Katika juhudi hizo Chuo kikuu cha Teknolojia cha Serikali cha Meru nchini Kenya kimevumbua mfumo wa kidigitali unaofahamika kama CovIdent utakaotoa alama za data binafsi kwa lengo la kurahisisha upimaji wa virusi vya corona kwa watu wengi.

Uvumbuzi huu umefanywa na wahandisi vijana chuoni hapo wanaotambulika kama NaiTech chini ya usimamizi wa mhandisi Bundi Kotonya.

**Mfumo huu unaweza kutambua maeneo yote ulikoenda na watu uliokutana nao, hivyo unapopata taarifa zote hizi inakua rahisi kudhibiti maambukizi zaidi.**

Mfumo huo utasaidia kuwapa watu nafasi ya kupata, kunakili na kutumia matokea ya upimaji wao kwa njia rahisi.

Mfumo huu utasaidia kuwatambua na kuwachuja wenye maambukizi ya virusi vya corona na hivyo kupunguza kuenea kwa virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Imeelezwa kuwa baada ya mtu kufanyiwa vipimo vya corona mfumo utaweka alama maalumu ya siri (code) na kutuma maelezo yake katika kituo cha taifa cha udhibiti wa corona au ugonjwa mwingine ambapo maelezo hayo yatahifadhiwa.


Prof. Romanus Odhiambo, aliyeongoza mpango wa uvumbuzi wa CovIdent, alisema alama hiyo ya kidigitali mtu anaweza kuitumia popote kuonyesha hali ya kiafya kuhusiana na corona na kuongeza kuwa unapotaka kwa mfano kuitumia kazini au mahala pengine, unapohitajika kutambulisha afya yako kuhusu corona mfumo wa CovIdent utakutambulisha kwa njia ya alama ya siri.

CovIdent unaweza kutambua mtandao wa watu ambao mtu amekutana nao, hivyo kutambua wagonjwa na watu wenye uwezekano wa kuambukizwa virusi vya corona baada ya kukutana na mtu mwenye maambukizo.

"Mfumo huu unaweza kutambua maeneo yote ulikoenda na watu uliokutana nao, hivyo unapopata taarifa zote hizi inakua rahisi kudhibiti maambukizi zaidi," alisema Mhandisi Bundi Kotonya, kiongozi wa vijana wavumbuzi CovIdent, katika Chuo Kikuu cha Meru.

Kwa mujinu wa Chuo Kikuu cha Meru, mfumo huo umebuniwa kwa ajili ya kuimarisha vita dhidi ya Covid-19, kwa kupunguza kuenea kwa virusi hivyo nchini Kenya na Afrika kwa ujumla.

Pamoja na CovIdent inaweza kuweka kutambulisha data za mtu binafsi za matibabu, chuo hicho kinatumaini unaweza kusaidia kutumika kutunga sera za afya duniani hususan kuhusiana na magonjwa ya maambukizi. **BBC**



Vijana walioshiriki utafiti katika Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Meru, nchini Kenya na kuvumbua mfumo wa CovIdent, ambao unaweza kusaidia kutumika kutunga sera za afya duniani. **PICHA: BBC**

## Hofu ya corona kuikumba Ikulu

**NEWYORK,** Marekani

MSEMAJI wa Makamu wa Rais wa Marekani, Mike Pence, ambaye ni mke wa mmoja kati ya washauri wakuu wa Donald Trump, amethibitishwa kuwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Hali ambayo inazua wasiwasi wa kusambaa kwa virusi hivyo katika Ikulu ya White House.

Rais Trump mwenyewe alitangaza Ijumaa wakati wa mkutano na wabunge na maseneta kutoka chama cha Republican, kwamba Katie Miller, mke wa mshauri wake katika masuala ya uhamiaji, Stephen Miller, ameathirika.

Kesi nyingine iliripotiwa siku moja kabla kati ya wafanyakazi wa White House wanaomhudumia Rais Trump.

Kwa mujibu wa mjumbe mashuhuri wa utawala wa Marekani, akinukuliwa na waandishi wa habari, Donald Trump na Mike Pence hivi karibuni hawakuweza kukaribiana na Katie Miller.

Trump na Pence wote wamepimwa na hawajapatikana na virusi vya corona hasa baada ya ofisa mmoja wa jeshi la Marekani anayehudumu katika Ikulu ya White House kuthibitishwa kuwa na virusi hivyo, ofisi ya rais wa Marekani ilisema. **RFI**

## Ufaransa na Hispania sasa kulegeza masharti karantini

**PARIS,** Ufaransa

UFARANSA na Hispania zinatarajia kulegeza masharti ya karantini yaliyowekwa kwa ajili ya kupunguza maambukizo ya virusi vya corona, huku idadi ya watu walioambukizwa virusi hivyo ikifikia milioni nne ulimwenguni.

Raia wa nchi hizo mbili wanapojiandaa kuanza kufurahia kupunguzwa kwa sheria za kubakia majumbani katika nchi hizo mbili zilizoathirika vibaya na janga la corona. Idadi ya watu walioambukizwa duniani imefikia milioni nne na watu wapatao 277,000 wamefariki kutokana na virusi hivyo.

Hatua ya kulegezwa masharti ya karantini inayotarajiwa kuanza leo, imesababisha hisia tofauti, huku baadhi ya wakuu wa sehemu za biashara wakielezea hofu yao juu ya kufunguliwa tena maduka. Maya Flandin, meneja wa duka la vitabu katika mji wa Lyon, amesema ana jukumu kubwa la kulinda afya za wafanyakazi na wateja wao.

Maofisa wa Afya Ufaransa wametahadharisha kwamba janga hilo linaendelea kuwapo na maambukizo yanatokea na wamekumbusha juu ya hali ya dharura iliyoongezewa muda hadi Julai 10, mwaka huu.

Hata hivyo, maaofisa wa afya Ufaransa wamesema idadi ya watu 80 waliofariki Jumamosi ni ya chini ukilinganisha na idadi ya watu waliokufa tangu mapema Aprili. Ufaransa inajiandaa kupunguza marufuku kwa harakati za umma iliyowekwa wiki nane zilizopita.

Nchini Uhispania, karibu nusu ya idadi ya watu wataruhusiwa kutoka majumbani mwao leo na wataruhusiwa kukusanyika katika makundi madogo madogo tu. Migahawa itaweza kutoa huduma wakati nchi hiyo inapoanza kipindi cha mpito baada ya karantini kitakachoendelea chini ya uangalizi hadi Juni.

Hata hivyo, hofu ipo ya kuibuka tena kwa virusi vya corona ikiwa vizuizi hivyo vitaondolewa kwa haraka. Mamlaka imesema miji ya Madrid na Barcelona haitahusishwa na kulegezwa kwa masharti hayo katika awamu hii ya kwanza kutokana na miji hiyo kuwa ndio vitovu vya covid-19 nchini Hispania. Waziri Mkuu, Pedro Sanchez, amekumbusha kwamba virusi vya corona bado havijatokomezwa.


Marekani ambayo inaongoza kwa idadi kubwa ya vifo ulimwenguni, Rais wa nchi hiyo, Donald Trump, amekosolewa vikali na mtangulizi wake, Barack Obama, aliyeonekana kwenye mkanda uliovuja kwamba Trump hakuushughulikia vyema mgogoro huo na kusababisha hali ya sintofahamu.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Chuo Kikuu cha Johns Hopkins, hadi kufikia jana, zaidi ya watu 78,000 walikuwa wamekufa kutokana na COVID-19 nchini Marekani, huku watu zaidi ya milioni 1.3 wakiwa wameambukizwa virusi vya corona.

Karantini na kudorora kwa uchumi, kwa wakati huu, kumesababisha mamilioni ya watu kukosa ajira na hali ngumu inayoukabili ulimwengu. Hata hivyo, pamoja na ongezeko kubwa la vifo, nchi kadhaa za Ulaya zimeonyesha ishara za maendeleo mazuri kutokana na kuchukua hatua za polepole kuelekea katika hali ya kawaida licha ya kwamba safari hiyo bado ni ndefu.

Takwimu za uchumi wa dunia zinaonyesha kushuka kwa kiwango kikubwa katika kipindi cha karibu karne moja kutokana na janga la corona lililolazimisha biashara kufungwa na pia kuvuruga vibaya shughuli za usambazaji. **DW**

# NEVILLE AWAFUNGUKIA POGBA, FERNANDES



**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba na Bruno Fernandes (pichani) wana uwezo wa kutengeneza upatina "wa kuvutia zaidi" kwenye kiungo ndani ya Manchester United kama watakuwa tayari "kushirikiana", amesema Gary Neville.

Kiungo Fernandes raia wa Ureno amekuwa na mwanzo mzuri pale United baada ya kujiunga kwa dau la pauni milioni 67.6 wakati wa dirisha la Januari kabla ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Fernandes alifunga mabao matatu na kutoa pasi nne za mwisho kwenye mechi tisa katika mashindano yote, lakini hajacheza pamoja na Pogba, ambaye hajaingia dimbani tangu Desemba mwaka jana kutokana na kuwa majeruhi.

Na sasa mlinzi wa zamani wa 'Mashetani Wekundu' hao, Neville ana matumaini Pogba na Fernandes watatengeneza upatina mzuri zaidi.

Akijibu swali katika kipindi cha maswali na majibu kupitia mtandao wa Twitter, Neville alisema: "Wanaweza kuwa na upatina wa kuvutia zaidi kama wakiwa tayari kushirikiana na kusaidiana."

# Fabregas: Ligue 1 imemalizika haraka



**MONACO,** Ufaransa

NYOTA wa Monaco, Cesc Fabregas, anahisi msimu wa 2019-20 wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, umefutwa haraka zaidi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Klabu ya Paris Saint-Germain ilipewa ubingwa wa ligi hiyo, huku Amiens na Toulouse zikishushwa daraja baada ya msimu huo kufungwa mwezi uliopita, huku zikiwa zimebakia mechi 10 kwa kila timu.

Wakati Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ikijiandaa kurudi Mei 16, mwaka huu na Ligi Kuu za England, Serie A na LaLiga zikiwa njiani kutaka kurudi, Fabregas anaamini Ligue 1 ingetakiwa kusubiri kabla ya kufungwa.

"Yalikuwa maamuzi makubwa yaliyofanywa na naweza kuelewa kwa nini waliamua kufanya hivyo," alisema kiungo Fabregas akiiambia beIN SPORTS.

"Lakini pengine ilichukuliwa kwa haraka sana, hasa ukichukulia ligi nyingi kubwa bado zinajaribu kutaka kurudi. "Ingawa naelewa sababu zilizopo nyuma yake, lakini naona kwamba ilifanywa haraka zaidi kumalizwa kwa ligi hiyo."

# Maradona bora zaidi ya Messi - Cannavaro

**ROME,** Italia

DIEO Maradona ni mchezaji bora wa wakati wote na si nyota wa Barcelona, Lionel Messi, kwa mujibu wa Fabio Cannavaro.

Maradona na Messi wote wanachulikuwa kama wachezai bora zaidi na raia hao wa Argentina wamekuwa wakiibua mjadala kila wakati kuhusu mafanikio yao kwenye timu ya taifa.

Messi ameweka rekodi ya kutwaa Ballon d'Or mara sita, lakini mlinzi wa zamani wa Italia, Cannavaro anaamini Maradona ambaye alitwaa Kombe la Dunia mwaka 1986 ni bora zaidi.

"Namheshimu sana Messi. Kwa kizazi kipya yeye ni mmoja wa wachezaji bora kabisa, lakini Maradona ni tofauti kabisa kwa sababu soka la wakati wao lilikuwa tofauti na sasa," alisema Cannavaro – ambaye kwa sasa ni kocha wa klabu ya Guangzhou Evergrande inayoshiriki Ligi Kuu ya nchini China, baada ya kutwaa Kombe la Dunia na Italia mwaka 2006 – akiiambia Sky Sports.

"Maradona alibutuliwa sana, lakini alikuwa na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira na alikuwa na nguvu.

"Messi ni wa daraja la juu, lakini Maradona ni wa dunia nyingine kabisa. Siwezi kumlinganisha yeye na mchezaji mwingine. Sikuwahi kumuona Pele, lakini nimemwangalia Maradona, kwa miaka saba niliangalia kila mchezo aliocheza.

"Si mmoja wa wachezaji bora, bali ni mchezaji bora."

Maradona alishinda mataji akiwa na Barcelona, akibeba Kombe la Mfalme [Copa del Rey], Copa de la Liga na Supercopa de Espana.

Gwiji huyo ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 59, alikuwa alama ya klabu ya Napoli, ambako alishinda mataji mawili ya Serie A, pamoja na Kombe la Uefa, Coppa Italia na Supercoppa Italiana.

Messi ameshinda mataji 10 ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pale Barcelona, ingawa hajapata mafanikio kwenye timu ya Taifa ya Argentina.



# Simeone ni kocha wa maisha Atletico - Emery

**MADRID,** Hispania

UNAI Emery amesema kwamba, Diego Simeone amepata kazi ya maisha yake yote katika klabu ya Atletico Madrid.

Aidha, ameeleza kuwa, kama Simeone mwenyewe asipoamua kuachia nafasi hiyo pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano, Emery haoni uwezekano wa raia huyo wa Argentina kutimuliwa.

Emery amekuwa hana timu tangu alipotimuliwa katika Klabu ya Arsenal ambako alitua akitokea Paris Saint-Germain.

Simeone ametumia misimu zaidi ya nane akiwa kocha wa Atletico, akiwaongoza kutwaa taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu wa 2013-14 na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili.

Atletico wamejiimarisha wao wenyewe kama wapinzani wakubwa wa klabu za Real Madrid na Barcelona kwenye soka la nchini Hispania.

"Unakwenda kule wanakotaka," alisema Emery akiliambia gazeti la AS. "Kwa sasa naishi Valencia ili kuwa na mwanangu, lakini nimejiandikisha jijini Madrid. Lakini sijui kituo changu cha kwanza kitakachofuata kitakuwa wapi, nipo wazi kwa kila kitu.

"Kitu kilichopo wazi ni kwamba, Atletico wana Simeone, ambaye anaweza kuwa nao hadi pale yeye mwenyewe atakapoamua kuondoka. Kwa sababu hakuna anayefiti pale zaidi ya yeye."





# LIVER YAJIWEKA PAZURI KUMSAJILI KOULIBALY

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imeripotiwa kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili mlinzi wa Napoli, Kalidou Koulibaly.

Koulibaly mwenye umri wa miaka 28, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo, huku timu kadhaa kubwa za Ulaya zikiwania saini yake kwa udi na uvumba.

Na sasa inaonekana kwamba, Liverpool wapo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupata huduma ya Koulibaly ambaye atakwenda kuungana na Virgil van Dijk kwenye nafasi ya ulinzi pale katika dimba la Anfield. Liverpool wapo kwenye nafasi hiyo nzuri kumsajili Koulibaly baada ya Paris Saint-Germain kujitoa kwenye mbio za kumuwania beki huyo raia wa Senegal, kwa mujibu wa Le 10 Sport.

Huku Manchester United pia ikiwa imeripotiwa kumuwania beki huyo, lakini sasa kikosi cha Jurgen Klopp kinaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri, huku pia Newcastle United - ambayo ipo sokoni kuuzwa, imeonyesha nia ya kumuwania.

Mkataba wa Koulibaly pale Napoli unamalizika mwaka 2023 na ada yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 88.4.

# *Umtiti aipa pigo Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

SAMUEL Umtiti ameumia katika siku ya pili ya kuanza mazoezi katika klabu ya Barcelona kwenye kituo cha mazoezi cha Ciutat Esportiva.

Mlinzi huyo wa kati aliumia kigimbi cha mguu wa kulia wakati wa mazoezi, na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wamethibitisha.

Barca walirudi kwenye mazoezi Ijumaa baada ya wachezaji wote na benchi la ufundi kupimwa virusi vya corona kabla ya kuanza kwa mazoezi hayo.

Jumamosi, walitawanywa kwenye viwanja vitatu tofauti ili kujifua ikiwa ni maandalizi ya kurudi tena kwa Ligi Kuu ya nchini humo.

Timu zote za LaLiga zimepewa ruhusa na vifaa kwa ajili ya kuanza mazoezi kabla ya ligi hiyo kuendelea Juni baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Barca walikuwa wanaongoza kwa pointi mbili kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu dhidi ya Real Madrid kabla ya msimu huo kusimamishwa Machi mwaka huu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAJIPANGA KWA AUBAMEYANG

●●● Yaipa Arsenal tarehe ya mwisho, huku Barca, Inter Milan na PSG nazo...

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeweka tarehe ya mwisho wakati ikiangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror.

**Madrid imeripotiwa kuwa imeitaka Arsenal kufanya maamuzi juu ya majaliwa ya Aubameyang kufikia Juni 15, mwaka huu.**

Mkataba wa sasa wa Aubameyang unamalizika Juni 2021 na mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon bado hajafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na Arsenal.

Nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund hajaonyesha nia ya kutaka kubaki kwenye klabu hiyo yenye maskani yake jijini London na majaliwa yake bado hayajulikani.

Na sasa Real Madrid imeripotiwa kuwania kumsajili mshambuliaji huyo ambaye ndiye anayeongoza kwa ufungaji wa mabao katika kikosi cha Arsenal msimu huu.

Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, inadaiwa kwamba anataka mshahara mnono zaidi ili kuweza kusaini mkataba mpya Arsenal kwa sababu huo unaweza kuwa wa mwisho katika kipindi chake cha uchezaji.

Pamoja na Real Madrid, klabu za Barcelona, Inter Milan na Paris Saint-Germain pia zimetajwa kwamba zinawania saini ya nyota huyo.

Msimu uliopita Aubameyang alitwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwa kuibuka mfungaji bora kwenye Ligi Kuu ya England pamoja na nyota wa Liverpool, Sadio Mane na Mohamed Salah.

## ZISIKUPITE

### SPURS KINARA KWA MEUNIER

KLABU ya Tottenham Hotspur kwa sasa inaongoza dhidi ya Manchester United kwenye mbio za kuwania saini ya mlinzi wa kulia wa Paris St-Germain, Thomas Meunier raia wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun on Sunday)***

### DE GEA ATAFUTIWA MBADALA

MANCHESTER United wanafikiria mbadala wa David de Gea, licha ya golikipa huyo mwenye umri wa miaka 29, raia wa Hispania kusaini mkataba mpya wa miaka minne Septemba mwaka huu. ***(Sunday Mirror)***

### MARTINEZ AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inajiandaa kutuma ofa kwa Inter Milan kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Lautaro Martinez, lakini Barcelona na PSG pia zinamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sunday Express)***

### ATLETICO KUMUUZA TRIPPIER

KLABU ya Atletico Madrid inajiandaa kumuuza beki wake wa pembeni raia wa England, Kieran Trippier kwa pauni milioni 20, huku klabu yake ya zamani ya Burnley ikionyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sun on Sunday)***

### LIVER KWA KINDA MBRAZIL

LIVERPOOL wanajiandaa kutoa ofa kwa mshambuliaji kinda wa Brazil, Talles Magno mwenye umri wa miaka 17, ambaye anaichezea klabu ya Vasco de Gama yenye maskani yake jijini Rio de Janeiro.***(Daily Star Sunday)***

### SAKA ANUKIA ANFIELD

KLABU ya Liverpool inaweza kumsajili beki wa kushoto wa Arsenal, Bukayo Saka, wakati huu raia huyo wa Uingereza mwenye umri wa miaka 18, mazungumzo yake ya kusaini mkataba mpya yakiwa yamesimama pale Emirates. ***(Sun on Sunday)***

### NYOTA LIVER KUTUA LIGUE 1

KIUNGO wa Liverpool, Pedro Chirivella mwenye umri wa miaka 22, raia wa Hispania, atajiunga na klabu ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, ya Nantes wakati mkataba wake utakapomalizika pale Anfield kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Football 365)***

### RABIOT KUONDOKA JUVE

KIUNGO wa Juventus, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 25, yupo tayari kwenda Manchester United au Everton baada ya raia huyo wa Ufaransa kushindwa kupata namba kwenye kikosi cha 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin. ***(Corriere di Torino)***

### SPURS KUMSAJILI FRASER

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kumsajili winga wa Bournemouth raia wa Scotland, Ryan Fraser mwenye umri wa miaka 26, akiwa mchezaji huru wakati wa kipindi kinachokuja cha majira ya joto, amesema mshambuliaji wa zamani wa Spurs, Darren Bent. ***(Sunday Express)***

### WENGER NA UBINGWA LIVER

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amesema Liverpool mara zote watatambulika kama mabingwa wa Ligi Kuu ya England, hata kama msimu huu utafutwa. ***(Talksport)***

HABARI MICHEZO



MAUMIVU...

Wachezaji wa timu ya Kitunda FC wakiwa mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SINGIDA UTD YATAKA LIGI KUU BARA IFUTWE

**Na Saada Akida**

HUKU timu yake ikipewa nafasi kubwa ya kushuka daraja kutokana na kuburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Singida United, Ramadhan Nsanzurwimo, amesema kwa upande wake anaona ni bora ligi hiyo ifutwe msimu huu.

**Singida United ipo mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 15 zilizotokana na mechi 29 ilizocheza hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona 9 (COVID-19).**

Wiki iliyopita Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almas Kasongo, alisema endapo serikali itatoa baraka za kuendelea kwa michezo nchini wanatarajia Ligi Kuu kurejea mapema Juni mwaka huu, jambo ambalo Nsanzurwimo hataki kuona likitokea.

Akizungumza na Nipashe jana, Nsanzurwimo alisema haoni sababu ya kurejesha kwa Ligi Kuu mapema kabla ya ugonjwa wa COVID-19 kumalizika hasa kutokana na mazingira ya mchezo huo ulivyo ambapo wachezaji hucheza na kufikia hatua ya kugusana na kutokuwapo kwa umbali unaotakiwa.

"Kwa upande wangu naona bora ligi ifutwe, hakuna bingwa wala kushuka daraja, mwakilishi wa kimataifa atachukuliwa yule bingwa wa Ligi Kuu na FA wa msimu uliopita," alisema kocha huyo.

Alisema endapo TPLB watashindwa kufuata, hivyo wasubiri janga hilo liishe na baadaye kupata muda wa makocha kuandaa timu zao ili kurejea uwanjani kumalizia msimu.

"Kama ligi itarudi muda huu, itawalazimu TFF na Bodi kutoa muda wa mwezi mmoja au miwili kwa ajili ya timu kufanya mazoezi, kwa sababu sasa hivi hatuelewi kama wachezaji wetu wanafanya mazoezi ipasavyo," alisema.

Nsanzurwimo alisema pia suala la kucheza mechi bila mashabiki ni adhabu kubwa kwa wachezaji pamoja na timu kutokana na asilimia kubwa ya klabu hutegemea mapato ya mlangoni.

# JKU yamwangukia Dk. Shein Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), likieleza kuwa kurejea kwa Ligi Kuu visiwani hapa kunategemea na kauli ya serikali, Katibu wa timu ya JKU, Sadu Ujudi, amesema ipo haja ya ligi hiyo kuanza tena kutimua vumbi na bingwa atakayeiwakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa kujulikana kihalali.

Katikati ya wiki iliyopita Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi ya ZFF, Haji Issa Kidali, aliliambia Nipashe kuwa kwa sasa wanasubiri muongozo kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kujua ligi zote zitarejea tena ama la.

Lakini jana Ujudi, akizungumza na gazeti hili, yeye alisema haoni sababu ya ligi hiyo kufutwa kwa kuwa michezo iliyobaki inauwezo wa kuchezwa ndani ya mwezi mmoja na bingwa kujulikana.

Alisema kufutwa kwa ligi kama wanavyodaia baadhi ya wadau wa soka kutasababisha kupata mwakilishi wa michuano ya CAF ambaye hakustahili, hivyo ni vema ligi hiyo ikamaliziwa kwa kuchezwa mechi zilizobaki.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na ZFF waangalie namna ya kurejesha ligi hiyo uwanjani na ikiwezekana ichezwa bila hata mashabiki ili kumaliza msimu huu.

"Sisi hamu yetu kubwa ni kuona Ligi Kuu Zanzibar inarejea uwanjani, ili tuweze kupata bingwa kihalali kabisa, michezo yenyewe imebaki michache tena sisi JKU ndio tunamichezo mingi iliyobaki (mechi saba), hivyo hatuoni sababu ya kufutwa kwa ligi," alisema.

Aidha, katibu huyo amemwomba Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kuruhusu ligi hiyo kuendelea kuchezwa na kutoa mwongozo wa kuchezwa ligi hiyo kwa kuzingatia kanuni zote za masuala ya afya Ili kuendelea kujikinga na virusi vya corona ambavyo vimesababisha kusimama kwa ligi hiyo.

Timu ya JKU ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar ikiwa na alama 45 wakipishana pointi moja na kinara wa ligi hiyo timu ya KMKM ambayo ipo kileleni na alama zake 46.

## Yanga yatazama ilipojikwaa mara 3

**Na Saada Akida**

MAKAMU Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, amesema licha ya kutojua Ligi Kuu Bara itarejea au laa, wao wameshaanza mikakati ya kuboresha walipokosea hali iliyosababisha kukosa ubingwa kwa msimu mitatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwakalebela alisema mbali na usajili ambao watakaoufanya pia kuna mikakati waliyojiwekea kuona kikosi chao kinafikia malengo yanayotarajiwa.

Alisema kukosa ubingwa kwa misimu mitatu kumewafanya kuanza kujipanga mapema ikiwamo upande wa usajili pamoja kuweka mazingira mazuri ya timu yao kujiandaa kwa msimu ujao.

"Katika usajili tunaenda vizuri, mwalimu Luc Eymael ametoa mapendekezo yake na kufanyiwa kazi, lakini viongozi tunaangalia upungufu mwingine na utawala kufanyia kazi," alisema Mwakalebela.

Alisema kwa sasa wanaomba Mungu janga hili la corona liishe, na endapo ligi itarejea wamalize salama na kuendelea na mchakato wao kujipanga kwa msimu ujao.

Mwakalebela alisema muda huu wa likizo ya corona wanautumia kutafakari jinsi gani ya kufikia malengo yao kuhakikisha msimu ujao wanatwaa ubingwa.

Hadi ligi hiyo inasimama Yanga ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 51, ikizidiwa alama 20 na mabingwa watetezi, Simba walioko kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, huku Azam FC ikishika nafasi ya pili kwa pointi zao 54.

Michezo
Jumatatu Mei 11, 2020
Nipashe



Real yajipanga kwa Aubameyang UKURASA 22

NAPASHA...



Nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi, akifanya mazoezi binafsi ya viungo nyumbani kwake jijini Dar es Salaam katika kipindi hiki klabu yake ikiwa imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **NA MPIGAPICHA WETU**

## Kocha Azam FC asifu Fifa kumjibu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) juzi limepitisha kwa kauli moja wanachama wake kutumia wachezaji watano wa akiba kutoka watatu wa awali pindi Ligi Kuu mbalimbali zitakaporejea, Kocha Mkuu wa Azam FC, Mromania Aristica Cioaba amefurahishwa na shirikisho hilo kuendana sawa na wazo lake alilolitoa awali kwa Bodi ya Ligi Tanzania, TPLB.

Kabla ya Fifa kutoa pendekezo hilo na kisha kulipitisha wiki iliyopita, wiki mbili zilizopita, Cioaba alitoa wazo hilo kwa TPLB akieleza kuwa itakuwa vizuri Ligi Kuu itakaporejea timu kuruhusiwa kufanya mabadiliko ya wachezaji watano badala ya watatu ili kuwaepusha kupata majeraha ya mara kwa mara kwa kuwa wamekuwa nje kwa kipindi kirefu bila kucheza soka.

Ligi Kuu imesimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na agizo la serikali la kuzuia shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo baada ya kuibuka kwa janga la maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19) duniani, na bado haijajulikana ni lini itarejea.

Lakini mwanzoni mwa wiki hii Fifa nao walikuja na wazo hilo, na kutoa pendekezo hilo kwa Bodi ya Kimataifa ya Kandanda (IFAB) kuongezwa kwa idadi ya wachezaji wa kubadilisha kwenye mechi moja kutoka watatu hadi watano ili kuwapa nafuu makocha na wachezaji baada ya kutocheza muda mrefu kutokana na janga la corona.

Na Cioaba akizungumzia hatua hiyo ya Fifa kuja na wazo kama lake na kisha kulipitisha na kupokelewa kwa mikono miwili na TFF, alisema: "Ni wazo muhimu sana kwa sababu ni jambo la kawaida katika kuwalinda wachezaji. Nimefurahia nilikuwa na wazo zuri, ambalo Fifa nao wamekuja nalo."

# Lamine aomba miaka 2 Yanga

### ●●● Ataka kujifunga hadi 2023, uongozi wampelekea Eymael, atoa neno...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, akisema kuwa klabu hiyo iko katika mkakati kabambe wa kuisuka timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao, beki wao kisiki, Mghana Lamine Moro amenogewa klabuni hapo na kuomba 'kufungwa' kwa miaka miwili zaidi.

**Mwakalebela aliliambia Nipashe jana kuwa mkakati wao ni kuisuka klabu hiyo upya ili kujiuliza ni wapi walipojikwaa na kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa misimu mitatu mfululizo na wakati akiyasema hayo Lamine tayari ameomba kupewa mkataba wa miaka miwili zaidi ili kuwa sehemu ya mafanikio yajayo ya kikosi hicho.**

Akithibitisha Lamine kuomba kuongezewa mkataba wa miaka miwili kutoka mmoja aliobakiza, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema ni kweli beki huyo raia wa Ghana amewasilisha ombi hilo mezani kwao na kinachosubiriwa ni janga hili la corona kupita ili kukamilisha mchakato huo.

Bumbuli alisema, kimsingi Lamine amebakiza mkataba wa mwaka mmoja ambao unamalizika Julai 2021, lakini ameomba kuongezewa miaka miwili na tayari ombi hilo limefikishwa kwa uongozi na bila kuchelewa wakalifikisha kwa Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael ambaye ameridhia beki huyo kuongezewa mkataba.

"Ni kweli kama mlivyoona kupitia akaunti yetu ya klabu kwamba Lamine Moro anatarajiwa kuongezwa mkataba wa kuitumikia Yanga hadi 2023, ameomba yeye mwenyewe na tumewasiliana na kocha amependekeza aongezwe.

"Kocha amesema Lamine bado ni mchezaji kijana na ana nguvu na uwezo wa kuendelea kuitumikia klabu kwa muda mrefu zaidi, hivyo amemkubali, kilichobaki ni uongozi kukaa baada ya janga hili la corona kupita na kumwongezea mkataba," alisema Bumbuli.

Lamine ambaye amezaliwa Februari 13, 1994 Accra nchini Ghana, amekuwa msaada mkubwa katika safu ya ulinzi ya Yanga ambapo kabla ya Eymael kutua, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa alikuwa akimchezesha sambamba na Kelvin Yondani.

Hata hivyo, kutua kwa Eymael kulimfanya Yondani kupoteza namba kikosi cha kwanza na chaguo la Mbelgiji huyo likawa ni Juma Makapu na Lamine, ambao wamefanya kazi kubwa katika safu ya ulinzi ya timu hiyo ambayo imeruhusu mabao 20 tu kwenye mechi 27 ilizocheza wakati huu ikiwa na alama 51 katika nafasi ya tatu, ambazo ni pointi 20 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, watani zao, Simba.

Tayari Yanga imemwongezea mkataba winga mshambuliaji wao, Mghana Bernard Morrison, huku ikielezwa wamefikia hatua nzuri na kiungo wao mkabaji Mkongomani Papy Tshishimbi anayemaliza mkataba msimu huu.

Lakini tangu kusimama kwa Ligi Kuu Machi 17, mwaka huu kutokana na janga la corona, Yanga imekuwa ikihusishwa na usajili wa nyota kibao kutoka nje na ndani ya nchi.

Baadhi ya wachezaji ambao Yanga imekuwa ikihusishwa na kuhitaji huduma zao ni pamoja na kiungo wa Timu ya Taifa ya Rwanda (Amavubi) na Rayon Sports, Ally Niyonzima, kiungo mkabaji wa FC Kariobangi Sharks, Mkenya Yidah Sven, mshambuliaji Reliants Lusajo wa Namungo FC na beki wa kati wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >